# القرآن الحكيم

# QURANI TAKATIFU

Swahili Quran Translation

Juzuu - Five (Walmuhsanat)

by
Sheikh Abdullah Saleh Al-Farsy

الَّذِينَ مِنْ أَصْلَابِكُمْ وَأَنْ تَجْمَعُوا بَيْنَ الْأُخْتَيْنِ
إِلَّا مَا قَدْ سَلَفَ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٢٣﴾

madada wawili wakati mmoja; isipokuwa yale yaliyokwishapita. (Yaliyopita yamepita yasirejeshwe tena). Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Mwenye kurehemu(na) Mwenye kusamehe



وَالْمُحْصَنَاتُ مِنَ النِّسَاءِ إِلَّا مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ
كِتَابَ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَأُحِلَّ لَكُمْ مَا وَرَاءَ ذَٰلِكُمْ
أَنْ تَبْتَغُوا بِأَمْوَالِكُمْ مُحْصِنِينَ غَيْرَ مُسَافِحِينَ
فَمَا اسْتَمْتَعْتُمْ بِهِ مِنْهُنَّ فَآتُوهُنَّ أُجُورَهُنَّ
فَرِيضَةً وَلَا جُنَاحَ عَلَيْكُمْ فِيمَا تَرَاضَيْتُمْ بِهِ
مِنْ بَعْدِ الْفَرِيضَةِ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٢٤﴾

24. Na pia (mmeharimishiwa) wanawake wenye (waume zao) isipokuwa wale iliyowamiliki mikono yenu ya kuume. (Ndiyo) Sharia ya Mwenyezi Mungu juu yenu. Na mmehalalishiwa (kuoa wanawake) minghairi ya hawa. Muwatafute kwa mali zenu, kwa kuwaoa bila ya kufanya zina. Basi wale mnaowaoa miongoni mwao wapeni mahari yao yaliyolazimishwa. Wala si vibaya kwenu katika (kutoa) yale mliyoridhiana badala ya yale yaliyotajwa. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi(na) Mwenye hikima.

وَمَنْ لَمْ يَسْتَطِعْ مِنْكُمْ طَوْلًا أَنْ يَنْكِحَ الْمُحْصَنَاتِ
الْمُؤْمِنَاتِ فَمِنْ مَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ مِنْ فَتَيَاتِكُمُ
الْمُؤْمِنَاتِ وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِإِيمَانِكُمْ بَعْضُكُمْ مِنْ
بَعْضٍ فَانْكِحُوهُنَّ بِإِذْنِ أَهْلِهِنَّ وَآتُوهُنَّ

25. Na asiyeweza katika nyiye kupata mali ya kuoa wanawake waungwana Waislamu, (na aoe) katika wajakazi walio Waislamu iliyowamiliki mikono yenu ya kuume (ya kulia). Na Mwenyezi Mungu anajua sana imani yenu; nyinyi kwa nyinyi. (Watumwa na waungwana ni sawa sawa katika Uislamu). Basi waoeni kwa idhini ya mabwana wao na wapeni mahari yao kwa Sharia. (Waoeni na hali ya kuwa) ni wanawake wema wasiokuwa wenye

---

24. Hapa inabainishwa kuwa kila wanawake wasiokuwa wale waliotajwa ni halali kuwaoa. Na inatajwa kuwa lazima umpe mwanamke mahari yake yaliyotajwa wakati wa kuozwa. Lakini anasema vile vile Mwenyezi Mungu hapa kuwa mwenyewe mwanamke akikubali baadaye kumpunguzia mumewe yale mahari yaliyotajwa, basi khiari yake. Na mume akitaka kumwongezea yule mkewe zaidi kuliko mahari yaliyotajwa, pia khiari yake. Hayo mahari si bei ya mwanamke lakini ni zawadi tu—tunza—anayompa mkewe kuonyesha mahaba yake juu yake. Basi vipi siku ya kumwacha ukamwambia 'Nipe mwenyewe.'

25. Mtoto aliyezaliwa na mama aliye mtumwa wa watu anakuwa mtumwa wa hao masaidi (mabwana) zake mama yake japokuwa baba yake ni muungwana. Basi wanakatazwa hapa waungwana kuwaoa watumwa wa watu kwani watoto wao watakuwa watumwa.

Lakini akiwa mtu ni masikini, hana uweza wa kuoa mke muungwana — na anajiogopea kuzini—basi atapewa ruhusa kuoa huyo huyo mjakazi; asaa huyo bwana atakapomwona huyo mtoto, atamwonea huruma ampe uungwana. Na ndivyo wanavyohimizwa kufanya hivyo.

Tena wakaliwazwa hao masikini wanaooa wajakazi kuwa mazingatio kwa Mwenyezi Mungu ni dini — si nasaba. Na nyinyi katika dini ni wamoja — nyote Waislamu.

Lakini wanahimizwa waoe wake wazuri wasiozini ovyo ovyo wala kwa kinyumba. Katika zama zao za Ujahili mwanamke aliyekuwa akizini kwa kinyumba (na wanaume makhsusi) hawakuwa wakiona vibaya kumuoa. Wakiona vibaya kumuoa mwanamke aliyekuwa akizini na kila mpita njia. Basi katika Uislamu zinakatazwa zote zina mbili hizo na unaambiwa ujiepushe na kuoa wanawake waliokuwa na feli hizo; ila ikiwa wametubia kweli kweli, unaona kuwa hawataufanya mwendo huo tena.

Na ikatajwa hapa kuwa mjakazi (au mtwana) akizini atiwe nusu ya adabu anayotiwa muungwana. Muungwana anapigwa bakora 100; basi yeye atapigwa 50, kwani muungwana ana vizuwizi vingi vya kumzuia. Nidyo maana kama hakuzuilika atiwe adabu kubwa zaidi.

Na utumwa tumetaja katika Aya ya 177 ya *Suratul Baqarah* kuwa umekatazwa katika Uislamu ila kwa njia moja tu. Wakati wasiokuwa Waislamu wakiwapiga Waislamu, na Waislamu wakapigana nao, wakawa hao wasiokuwa Waislamu wanawafanya mateka Waislamu kuwa watumwa, basi na Waislamu nao watapata ruhusa kuwafanya mateka wa hao kuwa watumwa. Na wakitaka watawaachia bure wende zao kwao au wataachia kwa

kuzini na kila mtu wala si wenye kuzini na wanaume makhsusi (wa kinyumba). Na wanapoolewa kisha wakafanya ufasiki, basi itakuwa juu yao nusu ya adhabu iliyowekewa wanawake waungwana. Hayo (ya kuoa wajakazi wa watu) ni kwa yule miongoni mwenu anayeogopa kuzini. Na mkisubiri (msiwaoe mpaka mpate fedha za kuoa muungwana) ndio bora kwenu. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa Kusamehe (na) Mwingi wa Kurehemu.

أُجُورَهُنَّ بِالْمَعْرُوفِ مُحْصَنَٰتٍ غَيْرَ مُسَٰفِحَٰتٍ
وَلَا مُتَّخِذَٰتِ أَخْدَانٍ ۚ فَإِذَآ أُحْصِنَّ فَإِنْ أَتَيْنَ
بِفَٰحِشَةٍ فَعَلَيْهِنَّ نِصْفُ مَا عَلَى الْمُحْصَنَٰتِ مِنَ
الْعَذَابِ ۚ ذَٰلِكَ لِمَنْ خَشِيَ الْعَنَتَ مِنْكُمْ ۚ وَأَنْ
تَصْبِرُوا خَيْرٌ لَّكُمْ ۗ وَاللَّهُ غَفُورٌ رَّحِيمٌ ﴿٢٥﴾ ع

26. Mwenyezi Mungu anataka kukubainishieni na kukuongozeni katika mwendo wa wale waliokutangulieni, na (anapenda) kukukhafifishieni. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

يُرِيدُ اللَّهُ لِيُبَيِّنَ لَكُمْ وَيَهْدِيَكُمْ سُنَنَ الَّذِينَ
مِن قَبْلِكُمْ وَيَتُوبَ عَلَيْكُمْ ۗ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ ﴿٢٦﴾

27. Na Mwenyezi Mungu anataka kukukhafifishieni. Lakini wanaofuata matamanio (yao) wanataka mkengeuke mkengeuko mkubwa (uliokhalifu haki).

وَاللَّهُ يُرِيدُ أَن يَتُوبَ عَلَيْكُمْ وَيُرِيدُ الَّذِينَ
يَتَّبِعُونَ الشَّهَوَٰتِ أَن تَمِيلُوا مَيْلًا عَظِيمًا ﴿٢٧﴾

28. Mwenyezi Mungu anataka kukukhafifishieni maana mwanaadamu ameumbwa dhaifu (hana nguvu kubwa kabisa za kiwiliwili wala nguvu kubwa za kupigana na moyo na shetani).

يُرِيدُ اللَّهُ أَن يُخَفِّفَ عَنكُمْ ۚ وَخُلِقَ الْإِنسَٰنُ
ضَعِيفًا ﴿٢٨﴾

29. Enyi mlioamani! Msiliane mali zenu kwa batili. Isipokuwa iwe biashara kwa kuridhiana baina yenu. (Hiyo inajuzu) wala msijiue (wala msiue wenzenu). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kukuhurumieni.

يَٰٓأَيُّهَا الَّذِينَ ءَامَنُوا لَا تَأْكُلُوٓا أَمْوَٰلَكُم بَيْنَكُم
بِالْبَٰطِلِ إِلَّآ أَن تَكُونَ تِجَٰرَةً عَن تَرَاضٍ مِّنكُمْ ۚ
وَلَا تَقْتُلُوٓا أَنفُسَكُمْ ۚ إِنَّ اللَّهَ كَانَ بِكُمْ رَحِيمًا ﴿٢٩﴾

30. Na atakayefanya haya kwa uadui na dhulma, basi huyo tutamwingiza Motoni. Na hayo ni rahisi kwa Mwenyezi Mungu.

وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ عُدْوَٰنًا وَظُلْمًا فَسَوْفَ نُصْلِيهِ
نَارًا ۚ وَكَانَ ذَٰلِكَ عَلَى اللَّهِ يَسِيرًا ﴿٣٠﴾

31. Kama mkijiepusha na maovu makubwa mnayokatazwa, tutakufutieni makosa yenu madogo na tutakuingizeni mahali patukufu (kabisa. Napo ni Peponi).

إِن تَجْتَنِبُوا كَبَآئِرَ مَا تُنْهَوْنَ عَنْهُ نُكَفِّرْ عَنكُمْ
سَيِّـَٔاتِكُمْ وَنُدْخِلْكُم مُّدْخَلًا كَرِيمًا ﴿٣١﴾

---

vikomboleo. Si lazima kuwafanya watumwa. Yametajwa haya katika Aya ya 4 ya *Surat Muhammad* na huitwa *Suratul Qital.*

29. Hapa inakatazwa kuliana mali kwa njia za batili; inakubalishwa kuuziana kunakopatikana kwa ridhaa ya wote wawili—mwuzaji na mnunuaji. Basi na miamala mingine iliyokubalishwa katika Sharia itakuwa ni kama kuuziana.

Aliposema Mwenyezi Mungu 'Msijiue' imeingia kujiua mwenyewe mtu na kumwua mwenziwe kwani Waislamu wote ni kitu kimoja; na asiyekuwa mwislamu pia huna ruhusa kumuua.

Na katika tamko hili la Kuua inaingia kuua Khasa—akafa mtu mara moja. Na inaingia vile vile kufanya mambo ya kukuhilikisha kidogo kidogo mpaka ukahiliki; kama ulevi na maasi mengine kwani yote hayo yanahilikisha kidogo kidogo. Basi anayeyafanya hayo anaingia katika wanaojiua.

31. Hapa inasemwa kuwa tukijiepusha na ile midhambi mikubwa mikubwa Mungu atatusamehe vile vijidhambi vidogo vidogo, kwani binadamu muhali takriba kusalimika na hivyo vijidhambi vidogo.

Dhambi zote si namna moja. Kuna nyingine mateso yake madogo kwa kuwa dhara yake ni ndogo kwa mkabala wa hizo nyingine. Si kama zile dhambi kubwa kubwa kama:– (a) Kuua (b) Kwiba (c) Kula riba (na kila dhuluma) (d) Kulewa (e) Kuzini (au wanaume kwa wanaume wenyewe). Na kama haya.

32. Wala msitamani vile ambavyo Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yenu (kwa vitu hivyo) kuliko wengine. Wanaume wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma; na wanawake nao wanayo sehemu (kamili) ya vile walivyovichuma. Na mwombeni Mwenyezi Mungu fadhila Zake. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kila kitu.

وَلَا تَتَمَنَّوْا مَا فَضَّلَ اللَّهُ بِهِ بَعْضَكُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ ۚ
لِّلرِّجَالِ نَصِيبٌ مِّمَّا اكْتَسَبُوا ۖ وَلِلنِّسَاءِ
نَصِيبٌ مِّمَّا اكْتَسَبْنَ ۚ وَاسْأَلُوا اللَّهَ مِن فَضْلِهِ ۗ إِنَّ
اللَّهَ كَانَ بِكُلِّ شَيْءٍ عَلِيمًا ﴿٣٢﴾

33. Na kila watu tumewawekea jamaa (zao) wa kurithi yale waliyoyaacha wazazi wawili na jamaa. Na wale mliofungamana nao ahadi wapeni sehemu yao. Hakika Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kila kitu.

وَلِكُلٍّ جَعَلْنَا مَوَالِيَ مِمَّا تَرَكَ الْوَالِدَانِ وَالْأَقْرَبُونَ ۚ
وَالَّذِينَ عَقَدَتْ أَيْمَانُكُمْ فَآتُوهُمْ نَصِيبَهُمْ ۚ
إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ شَهِيدًا ﴿٣٣﴾

34. Wanaume (wawe) ni walinzi wa wanawake; kwa sababu Mwenyezi Mungu amewafadhilisha baadhi yao kuliko wengine, na kwa sababu ya mali zao wanazozitoa. Basi wanawake wema ni wale wenye kutii, wanaojihifadhi (hata) wasipokuwapo (waume zao); kwa kuwa Mwenyezi Mungu amewaamrisha wajihifadhi. Na wanawake ambao mnaona uasi wao kwenu waonyeni na waacheni peke yao katika vitanda na wapigeni. Na kama wanakutiini msiwatafutie njia (ya kuwaudhi bure). Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Aliye juu (na) Mkuu.

الرِّجَالُ قَوَّامُونَ عَلَى النِّسَاءِ بِمَا فَضَّلَ اللَّهُ
بَعْضَهُمْ عَلَىٰ بَعْضٍ وَبِمَا أَنفَقُوا مِنْ أَمْوَالِهِمْ ۚ
فَالصَّالِحَاتُ قَانِتَاتٌ حَافِظَاتٌ لِّلْغَيْبِ بِمَا حَفِظَ
اللَّهُ ۚ وَاللَّاتِي تَخَافُونَ نُشُوزَهُنَّ فَعِظُوهُنَّ
وَاهْجُرُوهُنَّ فِي الْمَضَاجِعِ وَاضْرِبُوهُنَّ ۖ فَإِنْ
أَطَعْنَكُمْ فَلَا تَبْغُوا عَلَيْهِنَّ سَبِيلًا ۗ إِنَّ اللَّهَ
كَانَ عَلِيًّا كَبِيرًا ﴿٣٤﴾

---

Si kama (a) Kumsema mtu kidogo (b) Kutazama lililoharimishwa, na kama hivi.

Basi ukijiepusha na makubwa, hivi vijidogo dogo vitasamehewa maadamu huvikithirishi.

Na katika mijidhambi mikubwa ni kuacha amri za Mwenyezi Mungu kama:– (a) Kuacha kusali (b) Kuacha kutoa zaka na misaada mingine (c) kuacha kufunga (d) Kuacha kuhiji (e) Kuacha kutazama wazee. Na kama haya.

Mara nyingi utasikia watu wakisema:– Kuwa baina ya mtu asiyesali wala kufunga wala . . . lakini hana ubaya na mtu. Na baina ya mtu anayeyafanya haya ya kusali na vyenziwe, na akawa anafanya na mabaya pia. Wanasema kuwa yule wa mwanzo ni afadhali bali ni bora khasa kuliko huyu. Lakini sivyo kabisa. Si bora wala si afadhali kuliko huyo wa pili yake kwani kule kuacha maamrisho ya Mwenyezi Mungu ni dhambi kubwa kabisa kama kule kufanya makatazo yake: bali wakati mwingine huko kuacha maamrisho kunakuwa ni dhambi zaidi.

32. Inakatazwa hapa watu kuhusudiana. Lakini inataka kila mtu ajitahidi afanye kama anavyofanya mwenziwe ili apate kama alivyopata huyo mwenziwe kama anataka; bila kumhusudu wala kumchukia, kwani hakukunyang'anya chako, sini. Kajitahidi na Mungu kampa. Na wewe jitahidi na Mungu atakupa. Mwombwa na Mtoa ni yule yule tu Rabana.

33. Hapo zamani mtu alikuwa akichukua mtoto wa watu akimlea na akimfanya kama wake—kwa kumrithi kila chake na kwa mengineyo. Na hutokana na wakwao, akawa hana ukhusiano nao, la kwa kurithiana wala mengine; ukhusiano wake huwa huku tu. Basi wanakatazwa hapa. Wanaambiwa kuwa kila mtu atarithiwa na jamaa zake sio na watoto wa kupanga au wazee wa kupanga. Hao watoto (au wazee) wa kupanga wanaweza kuwaandikia kitu katika mali yao. Lakini kisizidi thuluthi ya mali yao. Na kikipunguka kuliko thuluthi ndio bora zaidi. Au muradi wa tamko hili "Walladhyna Aqadat Aymaanukum" ni mke na mume. Mke anamrithi mume na mume anamrithi mke. Na bora kufasiri kwa hivi.

34. Hapa inaambiwa wanaume wawe ndio wenye amri juu ya wake zao—wawendeshe mwendo mzuri. Si kujifanya washupavu hao wanawake, hawataki kutii amri za waume zao. Ikiwa hivyo hawatakuwa Waislamu wa kweli. Hata mailimu ya sasa—*Biology* na nyinginezo—yanaonyesha wazi wazi kuwa wanaume wamewashinda wanawake katika kila kitu takriba.

Tena zimetajwa baadhi ya sifa za wanawake wazuri.

Khalafu ikatajwa adabu ya kutiwa wanawake wasiokuwa hivyo. Kwanza waonywe kwa maneno tu na waume zao. Yakiwa hayakufidi wawahujuru katika malazi—wasilale nao kitanda kimoja wala penginepo. Wakitoacha jeuri

35. Na kama mkijua kuwa kuna ugomvi baina ya mke na mume basi pelekeni mwamuzi mmoja katika jamaa za mwanamume na mmoja katika jamaa za mwanamke. Kama wakitaka mapatano Mwenyezi Mungu atawawezesha. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa habari za siri na habari za dhahiri.

وَإِنْ خِفْتُمْ شِقَاقَ بَيْنِهِمَا فَابْعَثُوا حَكَمًا مِّنْ
أَهْلِهِ وَحَكَمًا مِّنْ أَهْلِهَا إِن يُرِيدَا إِصْلَاحًا
يُوَفِّقِ اللَّهُ بَيْنَهُمَا إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلِيمًا خَبِيرًا ﴿٣٥﴾

36. Mwabuduni Mwenyezi Mungu wala msimshirikishe na chochote. Na wafanyieni ihsani wazazi wawili, na jamaa na mayatima na masikini na jirani walio karibu a jirani walio mbali, na rafiki walio ubavuni (mwenu) na msafiri aliyeharibikiwa, na wale iliyowamiliki mikono yenu ya kulia (kuume). Bila shaka Mwenyezi Mungu hawapendi wenye kiburi wajivunao

وَاعْبُدُوا اللَّهَ وَلَا تُشْرِكُوا بِهِ شَيْئًا وَبِالْوَالِدَيْنِ
إِحْسَانًا وَبِذِي الْقُرْبَىٰ وَالْيَتَامَىٰ وَالْمَسَاكِينِ
وَالْجَارِ ذِي الْقُرْبَىٰ وَالْجَارِ الْجُنُبِ وَالصَّاحِبِ
بِالْجَنبِ وَابْنِ السَّبِيلِ وَمَا مَلَكَتْ أَيْمَانُكُمْ
إِنَّ اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ مُخْتَالًا فَخُورًا ﴿٣٦﴾

37. Ambao hufanya ubakhili (wao) na huwaamuru watu (wengine) kufanya ubakhili (pia kama wanavyofanya wao), na wanayaficha aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa fadhila Zake. Na tumewaandalia makafiri adhabu ifedheheshayo.

الَّذِينَ يَبْخَلُونَ وَيَأْمُرُونَ النَّاسَ بِالْبُخْلِ
وَيَكْتُمُونَ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ مِن فَضْلِهِ وَأَعْتَدْنَا
لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿٣٧﴾

---

zao hata kwa hayo pia, basi wanapewa ruhusa waume wawapige wanawake hao pigo la kuwatisha, si la kuumiza.

Lakini Hadithi za Mtume zimebainisha kuwa bora asifikilie katika daraja hii ya kupiga. Ajitahidi kumtengeneza katika taa kwa ile adabu ya kwanza tu. Ikiwa hapana budi na kwa ile ya pili basi. Lakini asifike ile ya tatu.

Akishindwa yeye kutengeneza atie watu wawasuluhishe kwani Sulhu ndio kheri. Na hao watu inataka waingie wenyewe wasuluhishe hata kabla hawajaakiwa msaada wao, seuze wanapotakiwa.

Tena wanaonywa hapa hao wanaume wasiwafanyie jeuri wake zao bure kwa kujiona kuwa wao wakubwa. Mwenyezi Mungu Mkubwa kabisa zaidi juu yao. Na Ulamaa wengine wanafasiri "Haafidhaatun Lilghybi" kwa tafsiri hii: "Wawe wenye kuhifadhi siri zinazopita baina yao na waume zao na siri zinazopita majumbani mwao". Kwani mara nyingi wanawake wanakuwa waropokaji. Wazee wa kizamani wakisema kwa Kiswahili cha kizamani: "Mengi Hayarongwa" yaani 'pana mambo mengi kabisa ambayo HAIFAI kabisa kuyasema, seuze kuyatangaza." "Mambo ya nyumba kunga. Aibu kuyaeleza".

35. Wanaambiwa hapo hao waamuzi kama ikiwa kweli nia yao ni kupatanisha basi Mwenyezi Mungu atawasaidia mpaka yapatikane hayo mapatano ya kheri waliyoyakusudia—na Mwenyezi Mungu anajua nia ya kila mtu; hawezi kumficha. Basi wanahimizwa hapa watu wawe na nia nzuri na mapendeleo ya kheri juu ya wenziwao.

Na vile vile huyo mke na mume wanaambiwa wawe na nia nzuri ya kupatana kwani kupatana ndio kheri. Asiwe kila mmoja kashadidia aliposhadidia—hataki ila hilo alilokuwa akilitaka tu. Isiwe hivyo. Bali wasikilize maneno ya hao waamuzi ili wapate kupatana. Sharti kila mmoja aridhie kusamehe baadhi ya haki zake, sio kushikilia—ndindindi; habanduki alipo. Isiwe hivyo.

36. Wanaamrishwa watu hapa kumwabudu Mwenyezi Mungu tu peke yake na wamwombe Yeye tu peke Yake — Mwombwa Yeye tu Rabbana. *Iyyaka Naabudu Waiyyaaka Nastaiyn.* (Wewe tu peke Yako ndiye tunayekuabudu na Wewe tu peke Yako ndiye tunayekuomba msaada).

Na waamrishwa wawafanyie ihsani wazee na wengine hao waliotajwa hapo; hata wakiwa hawawakhusu 'Ndewe wala Sikio,' na hata wakiwa si Waislamu. Hata Waislamu wasiosoma wanajua hayo. Utawasikia wanasema 'Allah Allah Jirani Walau Kana Baniyani.' Basi ndivyo hivi Uislamu unavyosema.

Na huyo rafiki wa ubavuni mwenu ni yule unayekuwa naye sana, kame Mke (na jamaa zake), Mume (na jamaa zake), Rafiki, Unayefanya kazi naye pamoja, na kama hawa. Na huwa ndio mara nyingi mtu kuwasahau. Huenda kuwatafuta walio mbali akawasaidia akawasahau hawa walio ubavuni mwake. Ndio maana ikazidi kuhimizwa hapa. Wakamilishiwe hawa kwanza ndipo utoke nje. 'Mambo kwa daraja.' Inasemwa kwamba 'Kuweka kitu pasipokuwa mahala pake ni kama kudhulumu.' Basi kuwasaidia walio mbali ukawatupa walio karibu hakukupi thawabu; kutakupa dhambi kwani ni kudhuumu. Na mwisho wa Aya hii ya 36 mpaka mwisho wa Aya ya 38 wanatajwa watu wabaya asiowapenda Mwenyezi Mungu

38. Na ambao wanatoa mali zao kwa kuonyesha watu wala hawaamini (aliyoyasema) Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho. Na yule ambaye amekuwa Shetani ndiye rafiki yake, basi ana rafiki mbaya kabisa.

وَالَّذِينَ يُنْفِقُونَ أَمْوَالَهُمْ رِئَاءَ النَّاسِ وَلَا
يُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ وَلَا بِالْيَوْمِ الْآخِرِ ۗ وَمَنْ يَكُنِ
الشَّيْطَانُ لَهُ قَرِينًا فَسَاءَ قَرِينًا ﴿٣٨﴾

39. Na ingekuwa nini juu yao kama wangaliamini (aliyoyasema) Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho, na wakatoa katika yale aliyowapa Mwenyezi Mungu? Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema.

وَمَاذَا عَلَيْهِمْ لَوْ آمَنُوا بِاللَّهِ وَالْيَوْمِ الْآخِرِ وَ
أَنْفَقُوا مِمَّا رَزَقَهُمُ اللَّهُ ۚ وَكَانَ اللَّهُ بِهِمْ عَلِيمًا ﴿٣٩﴾

40. Hakika Mwenyezi Mungu hawadhulumu (viumbe vyake hata kitu kilicho sawa na) uzito wa mdudu chungu; na kama likiwa ni jambo jema (Yeye Mungu) atalizidisha na kutoa ujira mkubwa unaotoka kwake.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَظْلِمُ مِثْقَالَ ذَرَّةٍ ۖ وَإِنْ تَكُ حَسَنَةً
يُضَاعِفْهَا وَيُؤْتِ مِنْ لَدُنْهُ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٤٠﴾

41. Basi itakuwaje tutakapoleta shahidi katika kila uma; na tukakuleta wewe (Nabii Muhammad) uwe shahidi juu ya huu (uma wako)?

فَكَيْفَ إِذَا جِئْنَا مِنْ كُلِّ أُمَّةٍ بِشَهِيدٍ وَجِئْنَا بِكَ
عَلَىٰ هَٰؤُلَاءِ شَهِيدًا ﴿٤١﴾

42. Siku hiyo wale waliokufuru na kumwasi Mtume watatamani ardhi isawazishwe juu yao (yaani lau kuwa wamefukiwa tu kaburini bila ya kufufuliwa). Wala hawataweza kumficha Mungu hadithi yo yote (katika mambo waliyoyafanya).

يَوْمَئِذٍ يَوَدُّ الَّذِينَ كَفَرُوا وَعَصَوُا الرَّسُولَ لَوْ تُسَوَّىٰ
بِهِمُ الْأَرْضُ وَلَا يَكْتُمُونَ اللَّهَ حَدِيثًا ﴿٤٢﴾

43. Enyi mlioamini! Msikaribie Sala, hali mmelewa, mpaka myajue mnayosema, wala hali mna janaba — isipokuwa mmo safarini — mpaka mkoge. Na kama mkiwa wagonjwa (mmekatazwa

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا لَا تَقْرَبُوا الصَّلَاةَ وَأَنْتُمْ
سُكَارَىٰ حَتَّىٰ تَعْلَمُوا مَا تَقُولُونَ وَلَا جُنُبًا إِلَّا
عَابِرِي سَبِيلٍ حَتَّىٰ تَغْتَسِلُوا ۚ وَإِنْ كُنْتُمْ مَرْضَىٰ

---

Tafauti ya kibri na fakhri ni kuwa (a) Kibri huwa katika moyo — ukajiona nani kama wewe. Na yakijaa hayo katika moyo hudhihiri katika maneno — kwa kujisifu mwenyewe, kutukana wengine na kama haya. Na hudhihiri katika vitendo — kwa kuwatazama watu kwa jicho la kejeli, kutowabali wanapompitia wakamtolea salamu, kutowaendea katika shughuli zao na kama haya. Basi kibri kikifika daraja hii huitwa fakhri vile vile.

37. Kuficha aliyowapa Mwenyezi Mungu kama vile mtu kuwa na ilimu asiwafundishe watu — akafa nayo. Kama watu wengi walivyokuwa wakifanya zamani. Na wako wanaofanya mpaka sasa pia. Hawakubali kumfundisha mtu, au waiamfundisha mtu mmoja tu hivi au wawili watatu waliomkhusu kweli kweli, kwa kuona kuwa riziki yake itakatika, itachkuliwa na hao anaowafundisha. Wala sivyo, kwani kila mtu ana riziki yake, haizidi haipungui. Hata tukisema kuwa hataaniwa yeye tu sasa peke yake — wataendewa na hao wengine pia — basi iko nini? Si anajipatia thawabu kubwa kabisa za tangu uhai wake mpaka kufa kwake maadamu ilimu yake ile inaendelea kutumiwa? Kuna riziki kubwa zaidi kuliko hii itakayomfaa Akhera wala haitamdhuru Duniani? Lakini watu hawataki Akhera. Maangalizi yao ni kutazama tu dunia, kama alivyosema Mwenyezi Mungu kuwa "Bali nyinyi mnafadhilisha (starehe za) uhai wa dunia, na hali ya kuwa Akhera ndiyo bora na ndiyo ya kusalia milele."

38. Anayetaka alipwe hiyo Pepo na Mwenyezi Mungu basi sharti awe anafanya hayo mema yake kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, siyo kwa ajili ya kuwa watu wamwone wamsifu. Atakayefanya kwa nia hiyo hatakuwa na malipo yo yote Akhera; kwani kataka aonekane duniani, na kesha kuonekana.

40. Tazama rehma na huruma ya Mwenyezi Mungu juu ya viumbe: (a) wakifanya ovu moja hulipwa ovu moja, ikiwa hawakutubia; na husamehewa pindi wakitubia; na hwenda wakasamehewa bila ya kutubiá, na (b) wakifanya jema hulipwa chungu ya mema duniani na Akhera. Basi natujitahidi kufanya kila lilo jema; hata dogo kabisa hili tusilidharau kama tunavyoona hapa. Mtume akisema 'Jikingeni na Moto kwa kufanya mema japo kwa kutasadaki kwa kokwa moja tu hii ya tende.' Hapa ndipo pa kupandia ya kuvunia huko. Sharti tupande hapa ndio tukavune huko.

kutumia maji) au mmo safarini au mmoja wenu ametoka msalani (chooni) au mmewagusa wanawake — na msipate maji — basi ukusudieni (tayamamuni) udongo safi, mpake nyuso zenu na mikono yenu. Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye kurehemu na kusamehe (na) Mwenye kughufiria.

أَوْ عَلَىٰ سَفَرٍ أَوْ جَاءَ أَحَدٌ مِّنكُم مِّنَ الْغَائِطِ أَوْ لَامَسْتُمُ النِّسَاءَ فَلَمْ تَجِدُوا مَاءً فَتَيَمَّمُوا صَعِيدًا طَيِّبًا فَامْسَحُوا بِوُجُوهِكُمْ وَأَيْدِيكُمْ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَفُوًّا غَفُورًا ﴿٤٣﴾

44. Huwaoni wale waliopewa sehemu ya (kukifahamu) Kitabu (cha Mwenyezi Mungu Mayahudi na Manasara)? Wanakhiari upotofu (upotevu) na wanakutakieni mpotee njia (ya kheri).

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ يَشْتَرُونَ الضَّلَالَةَ وَيُرِيدُونَ أَن تَضِلُّوا السَّبِيلَ ﴿٤٤﴾

---

Atatamani kweli kweli mtu mwovu siku ya Kiama asiwe mwenye kufufuliwa, kwa kihoro atakachokiona, kama inavyosema Aya hii na zinavyosema Aya nyingine. Si kihoro hicho kitachowafika wabaya, wasijue pa kukimbilia.

43. Mpango wa kuharimishwa kulewa tumeutaja katika maelezo ya Aya ya 106 ya *Al Baqarah*, na katika maelezo ya 219 ya *Al Baqarah*.

Na imetajwa habari ya kutayamamu yaani kutumia mchanga badala ya maji katika (a) kutawadha, na (b) Kukoga.

Na kutumia kwenyewe unautumia (a) Usoni tu na (b) Mikononi.

Unapiga viganja vya mikono chini katika mchanga safi wenye vumbi. Khalafu unapaka uso wako kwa hilo vumbi jepesi lililomo katika hivyo viganja vya mkono. Na kama vumbi jingi, unalikumta kwanza.

Kisha unapiga tena viganja vyako vya mkono chini katika mchanga namna ule. Tena kwa mchanga uliomo katika kiganja cha kushoto unaupakapaka mkono wa kulia wote mpaka kifundoni kama unavyotawadha. Na kwa mchanga uliomo katika kiganja cha kulia unaupaka mkono wa kushoto kama vile ulivyofanya katika wa kulia.

Unafanya hivi unapotayamamu kuwa ni badala ya kutawadha, na unapotayamamu kwa kuwa ni badala ya kukoga. Kwa yote mawili kufanya kwenyewe ni hivi hivi.

*N.B.*—Kwa Kiibadhi na Kihanafi hufiki katika vifundo — unavipaka vitanga tu vya mikono. Kwa kiganja cha kushoto unapaka kitanga cha kulia; na kwa kiganja cha kulia unapaka cha kushoto.

Wamepotoa tafsiri ya Aya walioifanya ya 44, wamesema: "Hali mmelewa. Sio muradi wake kulewa ulevi maana ulevi umeharimishwa katika Uislamu. Kulewa huku ni kwa mtu kukosa kufahamu anayoyasema kama ilivyoeleza Aya yenyewe yaani kama mtu anakuwa na njaa au hasira au usingizi na mengineyo (Bukhari, Abu Dawud)."

Ujasiri wao katika kugeuza maneno ya Mwenyezi Mungu haukadiriki. Wao wanasema hapana Naskh kama tulivyowavunja katika Aya ya 106 ya *Al Baqarah*. Na Quran imejaa mifano ya kuonyesha Naskh kama hii—na tazama maelezo yetu katika Aya hii ya *Suratun Nisaa* na ile ya *Suratul Baqarah*. Basi ndio wanapindua tafsiri ya Aya hii ili usidhihiri ule uwongo wao wa kusema hapana Naskh. Wamekhiari kuyapindua maelezo na kugeuza tafsiri na kusingizia Hadithi za Mtume za Bukhari na Abu Daud. Wallahi! Waongo. Haikufasiriwa "Waantum Sukara" tafsiri hiyo waliyoitoa, la katika Hadithi zilizomo katika Bukhari wala Abu Daud wala za kitabu chingine chochote cha kutaja Hadithi wala katika tamko la mwanachuoni yo yote yule. Wao wametaja mwanzo wa tafsiri yao chungu ya vitabu vya tafsiri za kutegemewa ili kuonyesha kuwa wametegemea tafsiri hizo. Basi kwa nini hawakutaja kipi katika hivyo kilichofasiri tafsiri yao ya uwongo hii? Wanajua kwa yakini kuwa hamna humo. Wakaangukia kukisingizia kitabu cha Al Bukhari na Abu Daud. Kama huu si ukafiri ni kitu gani? Kwenda kugeuza muradi wa maneno ya Mwenyezi Mungu. Hii siyo kazi waliyofanya Mayahudi katika Taurati na Manasara katika Injili Wakalaaniwa na Mwenyezi Mungu. Basi anayetafuta laana itamfika.

44-46. Hapa unatajwa baadhi ya ubaya wa Mayahudi na Manasara. (a) Mayahudi na Manasara walikuwa wakibadili maneno yaliyo katika Taurati na Injili yanayoonyesha khabari za Nabii Muhammad au huyafasiri kwa namna nyingine ile yasimkhusu yeye wala yasikhusu habari ya Uislamu. (b) Walipokuwa wakija mbele ya Mtume (hasa Mayahudi) wakaambiwa maneno ya dini husema 'Tumesikia, tutafuata'; kumbe katika nyoyo zao wanasema "Tunaasi yote hayo unayoyasema, tunakudanganya tu." (c) Wanapokuja wakawasikia Masahaba wanapomsemesha. Mtume wakasema: *"Ismaa ghayra musmaa"* kama ada ya Waarabu ilivyokuwa. Waarabu walikuwa wanapomsemesha mtu wakasema: *Ismaa ghayra musmaa*. "Sikia, si mwenye kusikilizishwa Inshaallah"; yaani 'Si mwenye kusikilizishwa mabaya Inshaallah.' Basi wao Mayahudi wakimtamkia Mtume vivi hivi lakini wakidhamiria (wakikusudia) maana nyingine. Wakikusudia 'Si mwenye kusikilizishwa kheri Inshaallah — utakuwa ukisikia mabaya tu ya kukukereketa maisha yako.' (d) Wanapokuja hao Mayahudi wakawasikia Masahaba

45. Na Mwenyezi Mungu anawajua vyema maadui zenu. Na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi, na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa msaidizi.

وَاللَّهُ أَعْلَمُ بِأَعْدَائِكُمْ ۚ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَلِيًّا وَكَفَىٰ
بِاللَّهِ نَصِيرًا ﴿٤٥﴾

46. Miongoni mwa Mayahudi wamo ambao hubadilisha maneno kuyatoa mahali pake, na husema (midomoni mwao): "Tumesikia"; Na (nyoyoni mwao husema): "Tumeasi". (Na wanasema kumwambia Mtume): "Sikia bila kusikilizwa;" Na (hulitamka tamko la): *"Raainaa"* kwa kuzipotoa ndimi zao (hata igeuke maana yake) ili kuitukana dini. Na kama wao wangalisema, "Tumesikia na tumetii. Na usikie na utuangalie" (kwa tamko la *Undhurna* badala ya tamko la *Raaina),* ingalikuwa bora kwao na vizuri zaidi. Lakini Mwenyezi Mungu amewalaani kwa kufuru zao; basi hawaamini ila kidogo tu.

مِنَ الَّذِينَ هَادُوا يُحَرِّفُونَ الْكَلِمَ عَنْ
مَوَاضِعِهِ وَيَقُولُونَ سَمِعْنَا وَعَصَيْنَا وَاسْمَعْ
غَيْرَ مُسْمَعٍ وَرَاعِنَا لَيًّا بِأَلْسِنَتِهِمْ وَطَعْنًا
فِي الدِّينِ ۚ وَلَوْ أَنَّهُمْ قَالُوا سَمِعْنَا وَأَطَعْنَا
وَاسْمَعْ وَانْظُرْنَا لَكَانَ خَيْرًا لَهُمْ وَأَقْوَمَ وَ
لَٰكِنْ لَعَنَهُمُ اللَّهُ بِكُفْرِهِمْ فَلَا يُؤْمِنُونَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٤٦﴾

47. Enyi mliopewa Kitabu! Aminini tuliyoyateremsha yanayosadikisha yale yaliyo nanyi, kabla hatujazigeuza nyuso tukazipeleka kisogoni, au kabla ya kuwalani kama tulivyowalani watu (walioharibu utukufu) wa Jumaamosi. Na amri ya Mwenyezi Mungu lazima kufanywa.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ آمِنُوا بِمَا نَزَّلْنَا
مُصَدِّقًا لِمَا مَعَكُمْ مِنْ قَبْلِ أَنْ نَطْمِسَ
وُجُوهًا فَنَرُدَّهَا عَلَىٰ أَدْبَارِهَا أَوْ نَلْعَنَهُمْ كَمَا
لَعَنَّا أَصْحَابَ السَّبْتِ ۚ وَكَانَ أَمْرُ اللَّهِ مَفْعُولًا ﴿٤٧﴾

48. Hakika Mwenyezi Mungu hasamehe kushirikishswa; na husemehe yasiyokuwa haya kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu bila shaka amebuni dhambi kubwa.

إِنَّ اللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَنْ يُشْرَكَ بِهِ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ
ذَٰلِكَ لِمَنْ يَشَاءُ ۚ وَمَنْ يُشْرِكْ بِاللَّهِ فَقَدِ افْتَرَىٰ
إِثْمًا عَظِيمًا ﴿٤٨﴾

49. Huwaoni wale wanaojitakasa nafsi zao? Bali Mwenyezi Mungu humtakasa amtakaye (akamwafikia kufanya mema). Na hawatadhulumiwa hata kijuzi kilichomo ndani ya uwazi wa kokwa ya tende.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يُزَكُّونَ أَنْفُسَهُمْ ۚ بَلِ اللَّهُ يُزَكِّي
مَنْ يَشَاءُ وَلَا يُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٤٩﴾

---

wanamwambia Mtume *"Raaina"* yaani 'Tutazame watu wako kwa jicho la rehema.' Na wao hulitamka tamko hili hili lakini kwa kulipotoa kidogo hata likageuka maana yake. Linakuwa — kwa lugha ya Kiyahudi — 'Ewe mpumbavu!' Basi wakikusudia maana haya. Kama tamko la Kiarabu la "Mukibba" lilioko katika *Suratil Mulk* ambao maana yake "Mwenye kusinukia (kuangukaanguka)." Baadhi ya watu wanaofasiri uwongo hulitamka kwa Mimu Sakin, wakasema 'Mkiba' na wakalifasiri kwa maana hayo ya kuiba.

Basi Waislamu wakaambiwa wasilitumie hilo tamko la *"Raainaa";* bali walitumie tamko la *"Undhurna."* Na maana yake ni ile moja lakini haliwezi kupotoleka likawa matusi.

47. Wanahadidiwa hivi hao Mayahudi na wenziwao kuwa Mwenyezi Mungu atawafanyia hayo kama alivyowafanyia wale waliovunja hishima ya Jumaamosi, kama ilivyotajwa katika maelezo ya Aya ya 65 ya *Suratul Baqarah.*

49. Hao hao Mayahudi walikuwa wanadeka kwa ajili ya hao Mitume wao na wazee wao waliokuwa wema. Wakisema maadamu wao wana watu kama hao basi hapana khofu juu yao. Kila wanalolifanya Mwenyezi Mungu atawasamehe, hata likiwa baya vipi. Na wakijita wao kuwa wao ni vipenzi vya Mwenyezi Mungu na watoto wa vipenzi vya Mungu.

50. Tazama jinsi wanavyotunga uwongo juu ya Mwenyezi Mungu, na haya yatosha kuwa dhambi zilizo dhahiri (za kuwatia Motoni).

انظُرْ كَيْفَ يَفْتَرُونَ عَلَى اللَّهِ الْكَذِبَ ۖ وَكَفَىٰ
بِهِ إِثْمًا مُّبِينًا ﴿٥٠﴾

51. Huwaoni wale waliopewa sehemu ya (kufahamu) Kitabu (cha Mwenyezi Mungu)? Wanaamini masanamu na upotofu. Na husema juu ya wale waliokufuru kuwa hao wameongoka zaidi katika njia (ya haki) kuliko wale walioamini.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ أُوتُوا نَصِيبًا مِّنَ الْكِتَابِ
يُؤْمِنُونَ بِالْجِبْتِ وَالطَّاغُوتِ وَيَقُولُونَ لِلَّذِينَ
كَفَرُوا هَٰؤُلَاءِ أَهْدَىٰ مِنَ الَّذِينَ آمَنُوا
سَبِيلًا ﴿٥١﴾

52. Hao ndio Mwenyezi Mungu aliowalani. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemlani basi hutamwona kuwa na mwenye kumnusuru.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ لَعَنَهُمُ اللَّهُ ۖ وَمَن يَلْعَنِ اللَّهُ
فَلَن تَجِدَ لَهُ نَصِيرًا ﴿٥٢﴾

53. Au wanayo sehemu ya ufalme (wa Mwenyezi Mungu; basi wanahamaki kwa nini kupewa mtu kitu pasina amri yao)? Basi hapo wasingaliwapa watu hata tundu ya kokwa ya tende

أَمْ لَهُمْ نَصِيبٌ مِّنَ الْمُلْكِ فَإِذًا لَّا يُؤْتُونَ
النَّاسَ نَقِيرًا ﴿٥٣﴾

54. Au wanawafanyia watu husuda kwa yale aliyowapa Mwenyezi Mungu kwa ukarimu Wake? Basi tuliwapa (vile vile) watoto wa Ibrahimu Kitabu na hikima na tukawapa ufalme mkubwa.

أَمْ يَحْسُدُونَ النَّاسَ عَلَىٰ مَا آتَاهُمُ اللَّهُ
مِن فَضْلِهِ ۖ فَقَدْ آتَيْنَا آلَ إِبْرَاهِيمَ الْكِتَابَ
وَالْحِكْمَةَ وَآتَيْنَاهُم مُّلْكًا عَظِيمًا ﴿٥٤﴾

55. Basi kuna miongoni mwao walioyaamini haya, na wako miongoni mwao waliojiepusha nayo. Na Jahanam yatosha kuwa moto mkali wa kuwaunguza.

فَمِنْهُم مَّنْ آمَنَ بِهِ وَمِنْهُم مَّن صَدَّ عَنْهُ ۚ
وَكَفَىٰ بِجَهَنَّمَ سَعِيرًا ﴿٥٥﴾

56. Hakika wale waliozikataa Aya zetu, tutawaingiza katika Moto. Kila ngozi zao

إِنَّ الَّذِينَ كَفَرُوا بِآيَاتِنَا سَوْفَ نُصْلِيهِمْ نَارًا

---

Basi ndio wanatolewa maanani hapa wanaambiwa 'Huwaoni wanaojitakasa nafsi zao kwa maneno ya midomo yao tu bila ya kufanya yale ya kuwatakasa?' Basi na baadhi yetu sisi huyadekea haya, wakaona maadamu wanatokana na wakubwa au wana alaqa na wakubwa, basi hapana khofu huko Akhera, si kweli haya hata chembe.

51. Tamko la Jibti na Taghuti linatumika katika Uislamu kama tamko la Sheitani. Hutumika katika kila ibada isiyokuwa ya haki (ya Mwenyezi Mungu) na katika kila jambo lisilowafiki Sharia ya haki.

Mayahudi bughudha yao ilipozidi juu ya Uislamu walikwenda kufanya Uitifaki na Makureshi na Waarabu wengine ili wamshambulie pamoja, Mtume na watu wake — wawasagesage, asisalie yo yote. Basi hao wakubwa wa Kiyahudi walipofika huko kwenda kufunga huo uitifaki waliwasujudia masanamu waliokuwa wakiabudiwa na Waarabu—na hali wao ni *Ahlil Kitabu* wanajua kuwa ni ukafiri kufanya hivyo. Na wakawatilia nguvu katika mambo mengine (hao Makureshi) na wakawaambia kuwa mwendo wao wa dini yao ni bora kuliko mwendo wa dini aliyokuja nayo Nabii Muhammad — na hali ya kuwa wanajua kuwa hivyo sivyo hata chembe lakini basi tu wanataka wapate huo msaada wa Makureshi na Waarabu wengine ili wawasagesage Waislamu kwa hasadi yao tu basi na kuona uchungu kwa nini Nabii Muhammad kupata neema hiyo ya Utume, kama kwamba ufalme wa Mwenyezi Mungu ni wao, wamehamaki kwa nini akapewa mtu kitu pasina amri yao. Ndiyo Mungu anawasimanga kwa namna hiyo katika Aya ya 53.

53-54. Aya za kuonyesha kuwa yote hayo waliyokuwa wakiyafanya Mayahudi ni kwa ajili ya husuda tu; wanaona kwa nini Waislamu wapate hayo waliyoyapata. Hapana kitu kinachowatia tabuni watu, kikawazuilia kufuata ya haki kama hasadi. Ukimhusudu mtu basi hukubali kufuata lake japo hilo ndilo la haki na lenye manufaa dhahiri duniani na Akhera. Basi natutahadhari na sifa hii ili tufuate yaliyo ndiyo tustarehe huku na huko.

Na hii hasadi ni kitiba (sifa) cha zamani sana, kama ilivyotajwa hapa katika Aya ya 54 na ndicho kilichompelekea Iblisi kuwa *Shaytanir Rajym* na *Qatilun athym*, na chungu ya wengineo tunaowasikia katika Tarehe.

zitakapowiva, tutawabadilishia ngozi nyingine badala ya zile; ili wawe wanaonja (uchungu wa) adhabu (maisha). Hakika Mwenyezi Mungu ni Mwenye nguvu (na) Mwenye hikima.

كُلَّمَا نَضِجَتْ جُلُودُهُم بَدَّلْنَاهُمْ جُلُودًا غَيْرَهَا
لِيَذُوقُوا الْعَذَابَ ۗ إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَزِيزًا حَكِيمًا ﴿٥٦﴾

57. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, tutawaingiza katika Mabustani yapitayo mito mbele yake kwa kukaa humo milele. Humo watakuwa na wake waliotakasika (na kila machafu), na tutawaingiza katika vivuli vizuri kabisa.

وَالَّذِينَ آمَنُوا وَعَمِلُوا الصَّالِحَاتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنَّاتٍ
تَجْرِي مِن تَحْتِهَا الْأَنْهَارُ خَالِدِينَ فِيهَا أَبَدًا ۖ
لَّهُمْ فِيهَا أَزْوَاجٌ مُّطَهَّرَةٌ ۖ وَنُدْخِلُهُمْ ظِلًّا ظَلِيلًا ﴿٥٧﴾

58. Hakika Mwenyezi Mungu anakuamrisheni kuzirudisha amana kwa wenyewe (wanaozistahiki). Na mnapohukumu baina ya watu mhukumu kwa haki. Bila shaka mawaidha anayokutoleeni Mwenyezi Mungu ni mazuri sana. Hakika Mwenyezi Mungu ndiye Asikiaye (na) Aonaye.

إِنَّ اللَّهَ يَأْمُرُكُمْ أَن تُؤَدُّوا الْأَمَانَاتِ إِلَىٰ
أَهْلِهَا وَإِذَا حَكَمْتُم بَيْنَ النَّاسِ أَن تَحْكُمُوا
بِالْعَدْلِ ۚ إِنَّ اللَّهَ نِعِمَّا يَعِظُكُم بِهِ ۗ إِنَّ اللَّهَ
كَانَ سَمِيعًا بَصِيرًا ﴿٥٨﴾

59. Enyi mlioamini! Mtiini Mwenyezi Mungu na mtiini Mtume na wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyie (Waislamu wenzenu). Na kama mkikhitalifiana juu ya jambo lo lote basi lirudisheni kwa Mwenyezi Mungu na Mtume, ikiwa mnamwamini Mwenyezi Mungu na siku ya mwisho. Hiyo ndiyo kheri, nayo ina matokeo bora kabisa.

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا أَطِيعُوا اللَّهَ وَأَطِيعُوا الرَّسُولَ
وَأُولِي الْأَمْرِ مِنكُمْ ۖ فَإِن تَنَازَعْتُمْ فِي شَيْءٍ فَرُ
دُّوهُ إِلَى اللَّهِ وَالرَّسُولِ إِن كُنتُمْ تُؤْمِنُونَ بِاللَّهِ
وَالْيَوْمِ الْآخِرِ ۚ ذَٰلِكَ خَيْرٌ وَأَحْسَنُ تَأْوِيلًا ﴿٥٩﴾

60. Huwaoni wale wanaodai kwamba wameamini yale yaliyoteremshwa kwako na yaliyoteremshwa kabla yako? Nao wanataka wakahukumiwe kwa njia isiyowafiki Sharia; na hali wameamrishwa kukataa njia hiyo. Na Shetani anataka kuwapoteza upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ يَزْعُمُونَ أَنَّهُمْ آمَنُوا بِمَا أُنزِلَ
إِلَيْكَ وَمَا أُنزِلَ مِن قَبْلِكَ يُرِيدُونَ أَن يَتَحَاكَمُوا إِلَى
الطَّاغُوتِ وَقَدْ أُمِرُوا أَن يَكْفُرُوا بِهِ وَيُرِيدُ
الشَّيْطَانُ أَن يُضِلَّهُمْ ضَلَالًا بَعِيدًا ﴿٦٠﴾

---

56-57. Hapa yanatajwa malipo ya wabaya na malipo ya wema. Hii ni ada ya Qurani. Ikitaja malipo ya wabaya, mara hutaja malipo ya wema, na ikitaja malipo ya wema, mara hutaja malipo ya wabaya ili watu watanabahi kuwa mema yao na mabaya yao, sio kwa nasabu zao au mali yao au vyeo vyao. Akisema sana Mtume haya, na Qurani imekariri sana pia.

58. Kuna baadhi ya watu huwachiwa amana na mtu, akaja akafa wala hakuweka mashahidi — au shahada ile haina nguvu — basi hurushilia mbali. Isiwe hivyo. Sio Uislamu huo. Mwislamu sharti awe mwaminifu, hata juu ya wasiokuwa Waislamu.

59. Kila wenye kutawalishwa ukubwa inataka watiiwe maadamu wanayoyaamrisha ndiyo ndivyo. Ikiwa hapana mkubwa wa kutiiwa yatakuwa mambo ovyo ovyo na litakuwa fujo. Na Uislamu haupendi mambo ovyo ovyo wala haupendi dhulma na jeuri.

Basi wakubwa watiiwe maadamu wanaamrisha mambo yaliyo ndiyo. Wakiamrisha yaliyo siyo hapana ruhusa kutiiwa.

Na ikitokea mzozano — kuwa wao wakubwa wanaona ndivyo, na nyinyi mlio chini yao mnaona sivyo — basi itazamwe Mwenyezi Mungu au Mtume Wake Wamesema nini katika mfano wa jambo hilo. Ifuatwe hukumu ya Mwenyezi Mungu na Mtume. Likiwa linastahiki kufuatwa lifuatwe, na likiwa halistahiki lisifuatwe. Wala asishadidie tena huyo mkubwa kuwa "Naliwe tu"; japo sivyo Sharia inavyosema. Wala wasishadidie hao wafuasi kuwa "Haliwi tu;" japo ndivyo Sharia inavyosema. Mategemeo iwe Sharia ya Mwenyezi Mungu na Mtumewe.

60. Hii Aya ya 60 na zilizo baada yake zinataja hukumu ya kukataa kuhukumiwa Kisharia.

Na inaingia katika Aya hii (a) Mtu kwenda kuposa mahali; wazee wa waposwaji wakenda kwa mpiga bao kutazamia kwanza kama arusi hiyo itakuwa na kheri au itakuwa na shari. Akiwaambia ina kheri wakubali au

61. Na wanapoambiwa: "Njooni katika yale aliyoyateremsha Mwenyezi Mungu, na (njooni) kwa Mtume," utawaona wanafiki wanajiweka mbali nawe kabisa.

وَإِذَا قِيلَ لَهُمْ تَعَالَوْا إِلَىٰ مَا أَنزَلَ اللَّهُ وَإِلَى
الرَّسُولِ رَأَيْتَ الْمُنَافِقِينَ يَصُدُّونَ عَنكَ
صُدُودًا ﴿٦١﴾

62. Basi itakuwaje utakapowafikia msiba kwa sababu ya yale iliyotanguliza mikono yao? Kisha wakakujia wakiapa "Wallahi! Hatukutaka ila wema na mapatano."

فَكَيْفَ إِذَا أَصَابَتْهُم مُّصِيبَةٌ بِمَا قَدَّمَتْ
أَيْدِيهِمْ ثُمَّ جَاءُوكَ يَحْلِفُونَ بِاللَّهِ إِنْ
أَرَدْنَا إِلَّا إِحْسَانًا وَتَوْفِيقًا ﴿٦٢﴾

63. Hao ndio wale ambao Mwenyezi Mungu anayajua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi waachilie mbali, (lakini) uwape mawaidha na uwaambie maneno yenye taathira yatakayoingia katika nafsi (nyoyo) zao.

أُولَٰئِكَ الَّذِينَ يَعْلَمُ اللَّهُ مَا فِي قُلُوبِهِمْ فَأَعْرِضْ
عَنْهُمْ وَعِظْهُمْ وَقُل لَّهُمْ فِي أَنفُسِهِمْ قَوْلًا بَلِيغًا ﴿٦٣﴾

64. Na hatukumleta Mtume yo yote ila atiiwe kwa amri ya Mwenyezi Mungu. Na lau wangalikuja walipojidhulumu nafsi zao (kwa kwenda kuhukumiwa kwa njia isiyokuwa ya Sharia) wakaomba msamaha kwa Mwenyenzi Mungu, na (yeye) Mtume pia akawaombea msamaha, bila shaka wangemkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kupokea toba (na) Mwenye kurehemu.

وَمَا أَرْسَلْنَا مِن رَّسُولٍ إِلَّا لِيُطَاعَ
بِإِذْنِ اللَّهِ وَلَوْ أَنَّهُمْ إِذ ظَّلَمُوا أَنفُسَهُمْ جَاءُوكَ
فَاسْتَغْفَرُوا اللَّهَ وَاسْتَغْفَرَ لَهُمُ الرَّسُولُ لَوَجَدُوا
اللَّهَ تَوَّابًا رَّحِيمًا ﴿٦٤﴾

---

akiwaambia ina shari waikatae. Badala ya kufuata alivyosema Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu — Mtume Muhammad *Sallal Laahu Alayhi Wasallam* — alikuwa akisema kama mtu ana wasiwasi wa jambo alifanye au asilifanye, basi asali rakaa mbili. Na mwisho wa sala katika *Tahiyyatu*—kabla ya kutoa salamu au baada ya kutoa salamu — asome dua hii na alitaje jambo lake hilo linalomfanyia wasiwasi; amwombe Mwenyezi Mungu amwafikie kulifanya kama likiwa na kheri na amwepushe nalo kama lina shari.

Ikiwa anaisoma dua hii ndani ya sala basi sharti aisome kwa Kiarabu. Ama akiisoma baada ya sala anaweza kuisoma kwa lugha aitakayo.

Ajitahidi asali kwa ukamilifu barabara na unyenyekevu uliokamilika. Basi akae siku moja mbili. Akiona moyo wake umelipenda jambo hilo basi nalifanye. Na akiona moyo wake umelichukia basi nasilifanye. Ukitomili moyo wake upande huu wala upande huu nasali tena mpaka imjie raghba ya mojapo—kulipenda au kulichukia.

Dua yenyewe kwa Kiswahili chake, ikiwa unaisoma baada ya kutoa salamu ni hii: "Ee Mola wangu! Mimi nakuomba unijulishe lililo la kheri kwa ujuzi Wako. Na nakutaka uniwezeshe (hilo la kheri) kwa uweza Wako. Na nakuomba unipe (hilo la kheri) kwa fadhila yako iliyo kubwa. Kwani wewe ndiye unayeliweza hilo mimi siliwezi. Na wewe ndiye unayelijua hilo wala mimi silijui. Na wewe ndiye Mjuzi wa yote yaliyofichikana. Ee Mola wangu! Ikiwa unajua kuwa jambo hilo ni la kheri na mimi katika dini yangu na uhai wangu na katika mambo yangu ya sasa na yanayokuja, basi niwezeshe na unisahilishie na unitilie baraka. Na ikiwa unajua kuwa jambo hilo ni shari yangu katika dini yangu na uhai wangu na katika mambo yangu ya sasa na yanayokuja, basi liepushe na mimi, na mimi niepushe nalo. Unikadirie la kheri popote lilipo na uniridhishe nalo kwa rehema Yako."

Na inaingia vile vile katika Aya hii (b) Mtu kuwa mgonjwa (yeye au mtu wake) akenda kwa mpiga bao kutazamia labda katendewa, na nani aliyemtendea. Au (c) Kuibiwa akenda kwa mpiga bao kutazamia; kwani mambo ya kuwasadiki wapigaji bao yamekatazwa kabisa.

Na inaingia — dhahir shahir — kwa wale wanaokataa kuhukumiwa kwa Sharia ya Uislamu (maneno ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake) wakataka wahukumiwe kikanuni *(decree)* kama wanavyokataa Wakopeshaji Riba kuhukumiwa Kiislamu. Anayaona maneno ya Mwenyezi Mungu na ya Mtume Wake siyo ya haki — akaona kanuni ndiyo yenye hukumu ya haki — basi mtu huyo ni kafiri.

64. Basi hao waendeaji wapiga bao na hao wapiga bao wenyewe — na wengineo wabaya kama hao wanaokataa kuhukumiwa Kiislamu wakataka kuhukumiwa Kikanuni — wakitubia baadaye, kwa shuruti zake, Mwenyezi Mungu atawapokea.

65. Naapa kwa (haki ya) Mola wako. Wao hawawi wenye kuamini (kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitalifiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa.

فَلَا وَرَبِّكَ لَا يُؤْمِنُونَ حَتَّىٰ يُحَكِّمُوكَ فِيمَا
شَجَرَ بَيْنَهُمْ ثُمَّ لَا يَجِدُوا فِي أَنفُسِهِمْ حَرَجًا مِّمَّا
قَضَيْتَ وَيُسَلِّمُوا تَسْلِيمًا ﴿٦٥﴾

66. Na kama tungeliwalazimisha kwamba "Jiueni nafsi zenu, au tokeni katika nyumba zenu (mwende vitani au muhame kabisa)," wasingalifanya hayo isipokuwa wachache tu katika wao. Na kama wangalifanya waliyoambiwa ingalikuwa bora kwao na yangekuwa yanathibitisha zaidi (Uislamu wao).

وَلَوْ أَنَّا كَتَبْنَا عَلَيْهِمْ أَنِ اقْتُلُوا أَنفُسَكُمْ
أَوِ اخْرُجُوا مِن دِيَارِكُم مَّا فَعَلُوهُ إِلَّا قَلِيلٌ
مِّنْهُمْ ۖ وَلَوْ أَنَّهُمْ فَعَلُوا مَا يُوعَظُونَ بِهِ لَكَانَ
خَيْرًا لَّهُمْ وَأَشَدَّ تَثْبِيتًا ﴿٦٦﴾

67. Na (ingekuwa hivyo) tungewapa malipo makubwa kutoka kwetu

وَإِذًا لَّآتَيْنَاهُم مِّن لَّدُنَّا أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٦٧﴾

---

65. Watu wakikhitalifiana katika jambo kuwa linafaa au halifai basi nawarejee maneno ya Mungu na Mtume. Watazame wamesema nini katika jambo hilo. Ifuatwe hivyo walivyosema. Wala moyo wake usinyonge kwa kuona kuwa alivyotaka yeye sivyo alivyotaka Mtume. Bali asalimu amri mara moja. Aone aliyoyataka Mtume ndiyo ndiyo.

Kama vile wanawake kuona kuwa amri zao zimo katika mikono ya waume zao. Basi wasichukiwe. Waone ndiyo haki hiyo aliyopenda Mwenyezi Mungu. Au vile mwanamume katika kumtoza anayemwacha — bila ya kufanyiwa vihendo na huyo mwanamke — akaambiwa kuwa Mwenyezi Mungu na Mtume wamesema kuwa hapana ruhusa hayo. Basi asione uchungu. Asalimu amri. Aone ya Mwenyezi Mungu na Mtumewe ndiyo ndiyo.

Au kama wafanyaji Matanga na ada zake na Tahalili na Arubaini na yaliyo kama haya. Wakiambiwa kuwa Mtume sivyo alivyosema. Basi inataka mara moja waache na waridhie kwa furaha. Wasione kuwa maiti wao wanakoseshwa thawabu. Wao wanajua mambo ya kumletea thawabu maiti kuliko anavyojua Mtume? Yangekuwa kweli hayo yanamletea thawabu maiti Mtume angeyakataza akawaambia Masahaba zake wawambie watu kuwa siyo hayo?

Basi tumfanye Mtume ndiye muamuzi katika khitilafu zetu zote. Akishakusema yeye kitu iwe basi.

Wamepindua kwa khatari kabisa muradi wa Aya hii walioifanya kuwa ya 60. Wameona humo Mwenyezi Mungu kasema *"Waulil Amri Minkum"* (Wenye mamlaka juu yenu, walio katika nyinyi yaani Waislamu wenzenu). Wao kwa ajili ya kuwavuta Waislamu wamtii Mngereza — na tafsiri yao hii ilitoka 1953 zama za utawala wa Waingereza huku — wameandika hivi:- "Katika maana iliyopanuka zaidi maneno haya yanawakusanya hata wale wasio Waislamu walio na mamlaka juu ya Waislamu."

Tazama ukafiri wao. Kwa ajili ya kutaka kuifurahisha dola ya Kiingereza wanapindua maneno wazi ya Mwenyezi Mungu; wanayavungavunga. Na tamko la *"Minkum"* ambalo maana yake: "Walio miongoni mwenu," au "wanaotokana na nyiye" au "walio katika nyiye . . ." Wamelipindua kwa tamko la *"Fykum;"* wakasema: "kati yenu—wenye mamlaka kati yenu." Na wanaona hapo kuwa Mwenyezi Mungu hakutumia *Fykum;* katumia *Minkum.* Tazama wanavyomgeuzia Mwenyezi Mungu maneno yake kwa ajili ya kutaka kuwafurahisha makafiri ili wawatukuze katika nchi hizi na wawaweke! Khatari kubwa kabisa.

Tena wakazidisha uwongo wao wakasema: "Suna na Hadithi za Mtume s.a.w. zimeweka jambo hili wazi ya kuwa katika mambo ya kidunia Waislamu wawatii hata hao watawala wao wasiokuwa Waislamu. . ." Waongo kabisa wazandiki wao. Kwa nini hawakuzitaja Hadithi hizo — japo kuwa moja — na mahali zilipo? Ukafiri mkubwa huu kumsingizia Mwenyezi Mungu na Mtumewe wasiyoyasema. Hadithi mashuhuri kabisa ya Mtume "Sikilizeni na mtii hata akikutawaleni mtumwa. . ."; hakusema "hata akikutawaleni asiyekuwa Mwislamu." Nawatuonyeshe Hadithi hiyo—na kama hiyo—kama ipo. Hawataipata, kwani haiko Wanataka tu kuifurahisha dola ya Kiingereza ambayo Imekwisha Utema (Imekwisha kufa) pande hizi sasa. Hawakuyajua haya. Walikuwa wakilewalewa na neema yao ya wakati huo. Leo watakwimbia au wanaimba:—

Pete ile — Kwanza yalikuwa yangu
Kiivaa — Kadiri ya chanda changu
Zama sizo — Wanaivaa wenzangu

68. Na Tungewaongoza njia iliyonyoka (ya kuwafikisha Peponi).

وَلَهَدَيْنٰهُمْ صِرَاطًا مُّسْتَقِيْمًا ﴿٦٨﴾

69. Na wenye kumtii Mwenyezi Mungu na Mtume, basi hao watakuwa pamoja na wale aliowaneemesha Mwenyezi Mungu: Manabii na Masidiki na Mashahidi na Masalih (watu wema). Na uzuri ulioje (kwa mtu) watu hao kuwa rafiki (zake).

وَمَنْ يُّطِعِ اللّٰهَ وَالرَّسُوْلَ فَاُولٰٓئِكَ مَعَ الَّذِيْنَ اَنْعَمَ
اللّٰهُ عَلَيْهِمْ مِّنَ النَّبِيّٖنَ وَالصِّدِّيْقِيْنَ وَالشُّهَدَآءِ
وَالصّٰلِحِيْنَ ۚ وَحَسُنَ اُولٰٓئِكَ رَفِيْقًا ﴿٦٩﴾

70. Hiyo ni fadhila itokayo kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi wa kutosha; (hapana asilolijua).

ذٰلِكَ الْفَضْلُ مِنَ اللّٰهِ ؕ وَكَفٰى بِاللّٰهِ عَلِيْمًا ﴿٧٠﴾

71. Enyi mlioamini! Shikeni hadhari yenu (juu ya maadui zenu. Msikhadaike). Tokeni (kwenda vitani) makundi moja moja au tokeni nyote pamoja (kama atakavyokwambieni Mtume).

يٰٓاَيُّهَا الَّذِيْنَ اٰمَنُوْا خُذُوْا حِذْرَكُمْ فَانْفِرُوْا ثُبَاتٍ
اَوِ انْفِرُوْا جَمِيْعًا ﴿٧١﴾

72. Na wako katika nyinyi wanaokaa nyuma (wasende vitani, na huwakataza wenziwao wasende vitani). Na kama unakupateni msiba (kila mmoja) husema: "Mwenyezi Mungu amenineemesha ilivyokuwa sikuhudhuria pamoja nao."

وَاِنَّ مِنْكُمْ لَمَنْ لَّيُبَطِّئَنَّ ۚ فَاِنْ اَصَابَتْكُمْ مُّصِيْبَةٌ
قَالَ قَدْ اَنْعَمَ اللّٰهُ عَلَىَّ اِذْ لَمْ اَكُنْ مَّعَهُمْ
شَهِيْدًا ﴿٧٢﴾

73. Na ikikufikieni fadhila kutoka kwa Mwenyezi Mungu (kama kupata ngawira na kushinda), husema—kana kwamba haukuwa urafiki baina yenu na baina yake — (husema): "Laiti ningalikuwa pamoja nao nikapata kufaulu kukuu (huko)."

وَلَئِنْ اَصَابَكُمْ فَضْلٌ مِّنَ اللّٰهِ لَيَقُوْلَنَّ كَاَنْ لَّمْ
تَكُنْ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهٗ مَوَدَّةٌ يّٰلَيْتَنِىْ كُنْتُ مَعَهُمْ
فَاَفُوْزَ فَوْزًا عَظِيْمًا ﴿٧٣﴾

74. Basi nawapigane katika njia ya Mwenyezi Mungu wale wanaouza maisha (yao) ya dunia kwa (kununua) ya Akhera. Na anayepigana katika njia ya Mwenyezi Mungu kisha akauawa au akashinda, tutampa ujira mkuu.

فَلْيُقَاتِلْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ الَّذِيْنَ يَشْرُوْنَ الْحَيٰوةَ
الدُّنْيَا بِالْاٰخِرَةِ ؕ وَمَنْ يُّقَاتِلْ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ
فَيُقْتَلْ اَوْ يَغْلِبْ فَسَوْفَ نُؤْتِيْهِ اَجْرًا عَظِيْمًا ﴿٧٤﴾

75. Na mna nini hampigani katika njia ya Mwenyezi Mungu na (katika kuwaokoa) wale walio

وَمَا لَكُمْ لَا تُقَاتِلُوْنَ فِىْ سَبِيْلِ اللّٰهِ وَالْمُسْتَضْعَفِيْنَ

---

69. Kila watakaofanya mema wataingia Peponi. Na kila watakaoingia Peponi watakutana na wenziwao wa Peponi wachanganyike, katika baadhi za nyakati, japokuwa wako mahala mbali mbali kwa mnasaba wa daraja walizopewa kwa amali zao ambazo hazikuwa namna moja. Lakini juu ya hivi watakutana.

Miongoni mwa daraja zilizotajwa hapa ni daraja ya (a) Unabii (b) Usiddiqi (c) Ushahidi (d) Usalih.

Salih ni anayetekeleza haki za Mwenyezi Mungu zilizo juu yake na kutekeleza haki za viumbe wenziwe zilizo juu yake, kwa mwisho wa uweza wake; Na Shahidi ni anayefanya haya na akapata bahati ya kuuawa kwa ajili ya dini; Na Siddiqi ni kama yule Salih. Lakini anatekeleza kwa ukamilifu zaidi kabisa, kama vile daraja ya Sayyidna Abubakrinis Siddiq.

Na Unabii ni kupindukia mipaka ya Ubinaadamu kwenda Umalaikani.

Ukafiri wao wa kudai kuendelea Utume walioutia hapa katika Aya hii walioifanya kuwa ni ya 70 ndio ule ule walioutia katika Aya 7 ya *Suratul Faatiha*, tukawajibu kwa urefu hapo. Basi tazama jawabu yao huko usalimike na ukafiri wao mkubwa kabisa huu wa kumdaia Utume mtu wao huyo. Huo ni ukafiri dhahir.

72. Zinatajwa habari za wanafiki na hatari yao, basi tujiepushe nao.

75. Baada ya kuhama Mtume Makka walisalia baadhi ya Waislamu — wanaume na wanawake na watoto— wamedhibitiwa na jamaa zao na kufungwa ndindindi, hawawezi kukimbia wakaja Madina. Na wanadhiliwa na kutaabishwa kweli kweli.

مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَآءِ وَالْوِلْدَانِ الَّذِينَ يَقُولُونَ رَبَّنَآ
أَخْرِجْنَا مِنْ هَٰذِهِ الْقَرْيَةِ الظَّالِمِ أَهْلُهَا ۚ وَاجْعَل
لَّنَا مِن لَّدُنكَ وَلِيًّا ۚ وَاجْعَل لَّنَا مِن لَّدُنكَ نَصِيرًا ﴿٧٥﴾

dhaifu — katika wanaume na wanawake na watoto — ambao husema: "Mola wetu! Tutoe katika mji huu ambao watu wake ni madhalimu, na tujaalie tuwe tuna mlinzi anayetoka kwako, na tujaalie tuwe na wa kutunusuru anayetoka kwako."

الَّذِينَ آمَنُوا يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۖ وَالَّذِينَ كَفَرُوا
يُقَاتِلُونَ فِي سَبِيلِ الطَّاغُوتِ فَقَاتِلُوا أَوْلِيَآءَ
الشَّيْطَانِ ۖ إِنَّ كَيْدَ الشَّيْطَانِ كَانَ ضَعِيفًا ﴿٧٦﴾

76. Wale walioamini wanapigana katika njia ya Mwenyezi Mungu, lakini waliokufuru wanapigana katika njia ya Shetani. Basi piganeni na marafiki wa Shetani. Hakika hila za Shetani ni dhaifu.

أَلَمْ تَرَ إِلَى الَّذِينَ قِيلَ لَهُمْ كُفُّوا أَيْدِيَكُمْ وَ
أَقِيمُوا الصَّلَاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ ۚ فَلَمَّا كُتِبَ
عَلَيْهِمُ الْقِتَالُ إِذَا فَرِيقٌ مِّنْهُمْ يَخْشَوْنَ النَّاسَ
كَخَشْيَةِ اللَّهِ أَوْ أَشَدَّ خَشْيَةً ۚ وَقَالُوا رَبَّنَا لِمَ
كَتَبْتَ عَلَيْنَا الْقِتَالَ ۚ لَوْلَا أَخَّرْتَنَا إِلَىٰ أَجَلٍ
قَرِيبٍ ۗ قُلْ مَتَاعُ الدُّنْيَا قَلِيلٌ ۚ وَالْآخِرَةُ خَيْرٌ
لِّمَنِ اتَّقَىٰ وَلَا تُظْلَمُونَ فَتِيلًا ﴿٧٧﴾

77. Huwaoni wale walioambiwa: "Izuieni mikono yenu (na kupigana na makafiri mpaka ije amri ya kupigana)? Na (sasa) simamisheni Sala, na toeni Zaka (tu)." Na (baadae) walipolazimishwa kupigana, mara kundi moja katika wao liliogopa watu (makafiri) kama kumwogopa Mungu au kwa khofu zaidi. Na wakasema: "Mola wetu! Kwa nini umetulazimisha kupigana? Lau ungetuakhirisha mpaka muda kidogo hivi (ingekuwa vizuri)." Sema: "Starehe ya dunia ni ndogo. Akhera ni bora zaidi kwa hao wenye kumcha Mungu. Wala hamtadhulumiwa hata uzi ulio katika uwazi wa kokwa ya tende."

أَيْنَمَا تَكُونُوا يُدْرِككُّمُ الْمَوْتُ وَلَوْ كُنتُمْ فِي بُرُوجٍ
مُّشَيَّدَةٍ ۗ وَإِن تُصِبْهُمْ حَسَنَةٌ يَقُولُوا هَٰذِهِ مِنْ
عِندِ اللَّهِ ۖ وَإِن تُصِبْهُمْ سَيِّئَةٌ يَقُولُوا هَٰذِهِ مِنْ
عِندِكَ ۚ قُلْ كُلٌّ مِّنْ عِندِ اللَّهِ ۖ فَمَالِ هَٰؤُلَاءِ الْقَوْمِ
لَا يَكَادُونَ يَفْقَهُونَ حَدِيثًا ﴿٧٨﴾

78. "Po pote mlipo mauti yatakufikieni, na hata mkiwa katika ngome madhubuti." Na kama ukiwafikia wema (wale wanafiki na makafiri) wanasema: "Huu umetoka kwa Mwenyezi Mungu." Na ukiwafikia uovu husema: "Huu umesababika kwa ajili yako (wewe Muhammad)." Sema: "Yote yametoka kwa Mwenyezi Mungu." Basi wamekuwaje watu hawa? Hawawezi kufahamu maneno?

مَّا أَصَابَكَ مِنْ حَسَنَةٍ فَمِنَ اللَّهِ ۖ وَمَا أَصَابَكَ
مِن سَيِّئَةٍ فَمِن نَّفْسِكَ ۚ وَأَرْسَلْنَاكَ لِلنَّاسِ

79. Wema uliokufikia umetoka kwa Mwenyezi Mungu; na ubaya uliokufikia unatoka nafsini mwako. (Mwenyewe umefanya mambo hata yakakufika hayo). Nasi tumekupeleka kwa watu

---

Basi wanahimizwa Waislamu vikitokea vita wapigane kweli kweli na hao makafiri mpaka waweze kuwaokoa hao Waislamu wanaotaabishwa hivyo.

Basi Waislamu wa kweli wakayafuata haya. Wakapigana hata wakaitia Makka mikononi mwao. Akatawalishwa liwali wa Kiislamu akawatoa taabuni wale Waislamu waliokuwa wakitaabishwa na kuomba vile. Dua ilisibu baada ya amri kufuatwa.

76. Muradi wa Marafiki wa Shetani ni wale makafiri wanaopigana na Waislamu.

77. Baadhi ya Masahaba walipokuwa Makka na ikashtadi juu yao shida za makafiri walimtaka ruhusa Mtume wapigane na hao maadui zao. Mtume akawaambia "Sikuamrishwa kupigana na maadui. Nimeamrishwa kuvumilia. Basi natuvumilie vivi hivi mpaka tujue nini mwisho wake."

Basi wakanyamaza. Hata walipofika Madina wakakaa kiasi cha mwaka hivi, walipewa ruhusa sasa kupigana na wale wanaowapiga. Lakini baadhi ya Masahaba wengine walifanya woga wakaona "Ah! Ya nini mambo ya kupigana? Kwa nini hatustahmili kama tulivyostahmili mwanzo?" Lakini kustahmili huko kutadumu mpaka lini? Ikiwa mtu hendi vitani hafi? Ndiyo wanazidi kusimangwa hivyo katika Aya ya 78.

kuwa Mtume. Na Mwenyezi Mungu ni Shahidi wa kutosha. (Hapahitajiwi shahidi mwengine).

رَسُولًا ۚ وَكَفَىٰ بِاللَّهِ شَهِيدًا ﴿٧٩﴾

80. Mwenye kumtii Mtume amemtii Mwenyezi Mungu (kwani anayoyaamrisha Mtume yametoka kwa Mungu). Na anayekengeuka (anajidhuru mwenyewe). Hatukukupeleka wewe kuwa mlinzi juu yao; (wakipotea ulaumiwe wewe. La. Hatukufanya hivyo).

مَّن يُطِعِ الرَّسُولَ فَقَدْ أَطَاعَ اللَّهَ ۖ وَمَن تَوَلَّىٰ فَمَا
أَرْسَلْنَاكَ عَلَيْهِمْ حَفِيظًا ﴿٨٠﴾

81. Na wanasema: "Tunatii;" Lakini wanapotoka kwako kundi moja miongoni mwao hushauriana usiku kinyume cha yale wanayoyasema (hapo mbele yako). Na Mwenyezi Mungu anayaandika yote hayo wanayoshauriana. Basi waachilie mbali, na mtegemee Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mlinzi wa kutosha.

وَيَقُولُونَ طَاعَةٌ فَإِذَا بَرَزُوا مِنْ عِندِكَ بَيَّتَ
طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ غَيْرَ الَّذِي تَقُولُ ۖ وَاللَّهُ يَكْتُبُ
مَا يُبَيِّتُونَ ۖ فَأَعْرِضْ عَنْهُمْ وَتَوَكَّلْ عَلَى اللَّهِ ۚ
وَكَفَىٰ بِاللَّهِ وَكِيلًا ﴿٨١﴾

82. Hawaizingatii nini, hii Qurani? Na kama ingelitoka kwa asiyekuwa Mwenyezi Mungu bila shaka wangalikuta ndani yake khitilafu nyingi.

أَفَلَا يَتَدَبَّرُونَ الْقُرْآنَ ۚ وَلَوْ كَانَ مِنْ عِندِ غَيْرِ
اللَّهِ لَوَجَدُوا فِيهِ اخْتِلَافًا كَثِيرًا ﴿٨٢﴾

83. Na linapowafikia jambo lo lote la amani au la khofu hulitangaza. Na kama wangalilipeleka kwa Mtume na kwa wenye mamlaka kwao, wale wanaopeleleza (wanaojua kupima mambo) miongoni mwao wangalijua (kuwa hilo ni jambo la kutangazwa au si la kutangazwa). Na kama isingalikuwa fadhila ya Mwenyezi Mungu juu ya (wengi katika) nyinyi na rehema yake, kwa yakini mngalimfuata Shetani isipokuwa wachache tu (waliopata fadhila hiyo).

وَإِذَا جَاءَهُمْ أَمْرٌ مِّنَ الْأَمْنِ أَوِ الْخَوْفِ
أَذَاعُوا بِهِ ۖ وَلَوْ رَدُّوهُ إِلَى الرَّسُولِ وَإِلَىٰ أُولِي
الْأَمْرِ مِنْهُمْ لَعَلِمَهُ الَّذِينَ يَسْتَنبِطُونَهُ مِنْهُمْ ۗ
وَلَوْلَا فَضْلُ اللَّهِ عَلَيْكُمْ وَرَحْمَتُهُ لَاتَّبَعْتُمُ
الشَّيْطَانَ إِلَّا قَلِيلًا ﴿٨٣﴾

---

81. Wanahadidiwa wanafiki kuwa Mungu anawaona na atawalipa.

82. Basi wanaiona hii Qurani maneno yake sawa sawa, hayapingani wala hawezi kiumbe kuleta hoja ya kuonyesha kuwa baadhi ya hayo yaliyosemwa humo ni uwongo—sivyo. Hakijatokea kitabu hicho wala hakitatokea. Kupinga kwa hoja na dalili khasa hakupatikani. Katika yaliyosemwa na Qurani ukadhihiri ukweli wake sasa ni: (1) Kuwa kila kitu kina Udume na Uke. Tazama Aya ya 36 ya *Surat Yasin;* (2) Kuwa dunia hii ilikuwa imekamatana na mbingu (kipande cha jua), kama ilivyo katika Aya ya 30 ya *Suratul Anbiyaa;* (3) Kuwa Uhai unategemea maji, kama ilivyo katika Aya ya 30 ya *Suratul Anbiyaa;* (4) Kuwa watu walio masafa mbali kabisa wataweza kusikilizana na wa masafa mbali kabisa, kama ilivyo katika Aya ya 44 ya *Suratul Aaraf;* (5) Kuwa watu wa masafa mbali sana wataweza kujuana, kama ilivyo katika Aya ya 46 ya hii hii *Suratul Aaraf* na nyinginezo; (6) Kuwa watu wa masafa mbali mbali wataweza kupeana vitu na kupokeleana, kama ilivyo katika Aya ya 50 ya hii ya *Suratul Aaraf;* (7) Kuwa watu watafika mbinguni, kama ilivyo katika Aya ya 13 ya *Suratul Jaathiya.*

Na mengi kabisa mengineyo.

Hapa katika Aya hii walioifanya kuwa ni ya 83 makadiyani wametaja habari ya Nasikh na Mansukh, kwa kuonyesha kuwa tukikubalisha Naskh, maneno ya Mwenyezi Mungu yatakhitalifiana yapingane. Wala sivyo. Hapatakuwa kukhitalifiana wala kupingana, bali itapatikana kuonekana wazi wazi hikima ya Mwenyezi Mungu na uwongozi wake mzuri wa kuwavuta watu kidogo kidogo. Tumeyabainisha haya katika Aya ya 106 ya hiyo *Suratul Baqarah.*

83. Wanakatazwa hapa watu kutangaza mambo yaliyokhusu siasa ya dola. Wasiyaseme ila yale yaliyosemwa na hao wakubwa, kwani wao ndio wanaojua yapi yanafaa kusemwa na yapi hayafai kusemwa.

84. Basi pigana katika njia ya Mwenyezi Mungu. Hukalifishwi ila nafsi yako. Na wahimize Waislamu. Huenda Mwenyezi Mungu akazuia mashambulio ya waliokufuru. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mkali wa kushambulia na Mkali wa kuadhibu.

فَقَاتِلْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ لَا تُكَلَّفُ إِلَّا نَفْسَكَ
وَحَرِّضِ الْمُؤْمِنِينَ ۚ عَسَى اللَّهُ أَن يَكُفَّ بَأْسَ
الَّذِينَ كَفَرُوا ۚ وَاللَّهُ أَشَدُّ بَأْسًا وَأَشَدُّ تَنكِيلًا ﴿٨٤﴾

85. Atakayeombea maombezi mema (atakayesaidia mambo mema hata yakatokea) atapata sehemu katika hayo. Na atakayeombea maombezi mabaya atakuwa na sehemu katika mabaya hayo, na Mwenyezi Mungu ni Mwenye ujuzi juu ya kila kitu.

مَّن يَشْفَعْ شَفَاعَةً حَسَنَةً يَكُن لَّهُ نَصِيبٌ مِّنْهَا ۚ
وَمَن يَشْفَعْ شَفَاعَةً سَيِّئَةً يَكُن لَّهُ كِفْلٌ مِّنْهَا ۚ
وَكَانَ اللَّهُ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ مُّقِيتًا ﴿٨٥﴾

86. Na mnapoamkiwa kwa maamkio yo yote yale, basi itikieni kwa yaliyo bora kuliko hayo, au rejesheni yayo hayo. Hakika Mwenyezi Mungu anafanya hisabu ya kila kitu.

وَإِذَا حُيِّيتُم بِتَحِيَّةٍ فَحَيُّوا بِأَحْسَنَ مِنْهَا أَوْ رُدُّوهَا ۚ
إِنَّ اللَّهَ كَانَ عَلَىٰ كُلِّ شَيْءٍ حَسِيبًا ﴿٨٦﴾

87. Mwenyezi Mungu, hakuna anayestahiki kuabudiwa ila Yeye tu. Kwa yakini atakukusanyeni siku ya Kiyama. Hapana shaka ndani yake (Hakina shaka). Na nani mkweli zaidi katika maneno kuliko Mwenyezi Mungu?

اللَّهُ لَا إِلَٰهَ إِلَّا هُوَ ۚ لَيَجْمَعَنَّكُمْ إِلَىٰ يَوْمِ الْقِيَامَةِ لَا
رَيْبَ فِيهِ ۚ وَمَنْ أَصْدَقُ مِنَ اللَّهِ حَدِيثًا ﴿٨٧﴾

88. Imekuwaje nyinyi kuwa makundi mawili katika khabari ya wanafiki, na hali Mwenyezi Mungu amewageuza kwa sababu ya yale (mabaya) waliyoyachuma? Je! Mnataka kumwona mwongofu ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kuwa kapotea? Na aliyemhukumu Mwenyezi Mungu kuwa amekwisha potea hutampatia njia (ya kuambiwa mwongofu).

فَمَا لَكُمْ فِي الْمُنَافِقِينَ فِئَتَيْنِ وَاللَّهُ أَرْكَسَهُم
بِمَا كَسَبُوا ۚ أَتُرِيدُونَ أَن تَهْدُوا مَنْ أَضَلَّ اللَّهُ ۚ
وَمَن يُضْلِلِ اللَّهُ فَلَن تَجِدَ لَهُ سَبِيلًا ﴿٨٨﴾

---

84. Mtume anaambiwa kuwa juu yake ni kuamrisha na kuhimiza tu; lakini kukalifisha kwa nguvu si juu yake. Ataikalifisha kwa nguvu nafsi yake tu mwenyewe.

85. Wanaamrishwa watu kusaidia mambo ya kheri, kusaidia kwa vitendo na maneno—kuwavuta wenziwe, kama anavyoweza, wafanye na wasaidie mambo ya kheri; na watapata jaza kubwa kabisa wakifanya hivi, kwani kheri ndiyo inayotakiwa itapakae ulimwengu mzima.

Na wanakatazwa kabisa kabisa kusaidia ya shari hata kwa msaada mdogo kabisa hata wa neno dogo tu hili kulitia katika kusaidia jambo baya, japo kwa kulipigia kofi kulishangilia na kumshangilia aliyefanya, bali hata kwa kufurahi moyoni kwako tu. Baya inataka ujiepushe nalo kila namna.

Juu yako ni kuliondosha na kuwasaidia wanaoliondosha, sio kulisaidia au kuwasaidia wanaolifanya. Mwislamu ajiweke kuwa nafuu tu kwa viumbe wote wanaostahiki kunufaishwa (kunafiishwa). Kama huwezi kunufaisha, basi jizuilie na kudhuru.

86. Uislamu unahimiza kweli kweli kuanza kuwafanyia viumbe wema na kuwalipa vizuri kabisa wakikufanyia huo wema. Basi inasemwa hapa kuwa hata ukiamkiwa ujibu kwa vizuri zaidi kuliko alivyokuamkia. Akikwambia "*Saba hal Kheyr* (Subal Kheri)" mwambie kama hivi "Subalkheri Bwana au Bibi." Au "Shikamoo" "Shikamoo Bwana au Marhaba mwanangu." Akikwambia "*Assalam Alaykum*" mwambie "*Waalaykumus Salam wa Rahmatul Lah.*" Akisema "*Assalamu Alaykun wa Rahmatul Lah,*" mwambie "*Waalaykumus Salam wa Rahmatul Lahi wa Barakatuh.*" Na kama hivi. Fanya wema na usipunguze kulipa wema kwa wema zaidi kuliko alioku fanyia.

88. Tumeona kuwa katika siku ya vita vya Uhudi kiasi cha watu 300 walikimbia kwa siri wakamwacha Mtume na watu 700 tu wakabiliane na jeshi la watu 3000. Watu wengi waliwaitakidi watu hao kuwa makafiri. Lakini wengine waliwaitakidi ni Waislamu kwa vile wanavyojidai kusali na kufunga na mengineyo. Basi wanabainishiwa hapa dhahir shahir kuwa hao ni makafiri, si Waislamu. Kama wangelikuwa Waislamu

89. Wanataka (makafiri wa Kiarabu) lau mngekufuru kama walivyokufuru wao ili muwe sawa sawa. Basi msiwafanye wao marafiki (wa kuwapa siri zenu) mpaka wahame kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu (waje wakae Madina pamoja na nyinyi). Na kama wakikengeuka basi wakamateni na waueni po pote mnapowapata (kama wanavyokufanyieni hivyo). Wala msifanye rafiki katika wao wala msaidizi

وَدُّوا لَوْ تَكْفُرُونَ كَمَا كَفَرُوا فَتَكُونُونَ سَوَاءً فَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ أَوْلِيَاءَ حَتَّىٰ يُهَاجِرُوا فِي سَبِيلِ اللَّهِ ۚ فَإِنْ تَوَلَّوْا فَخُذُوهُمْ وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ ۖ وَلَا تَتَّخِذُوا مِنْهُمْ وَلِيًّا وَلَا نَصِيرًا ﴿٨٩﴾

90. Isipokuwa wale wanaopatana na watu ambao mna ahadi baina yenu na wao, au wajao kwenu, na vifua vyao vinaona dhiki kupigana nanyi au kupigana na watu wao. (Hao msiwapige). Na kama Mwenyezi Mungu angalipenda angezitia nguvu nyoyo zao juu yenu wakapigana nanyi. Na kama wakijitenga wasipigane nanyi na wakakuleteeni amani, basi Mwenyezi Mungu hakukufanyieni njia juu yao.

إِلَّا الَّذِينَ يَصِلُونَ إِلَىٰ قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُمْ مِيثَاقٌ أَوْ جَاءُوكُمْ حَصِرَتْ صُدُورُهُمْ أَنْ يُقَاتِلُوكُمْ أَوْ يُقَاتِلُوا قَوْمَهُمْ ۚ وَلَوْ شَاءَ اللَّهُ لَسَلَّطَهُمْ عَلَيْكُمْ فَلَقَاتَلُوكُمْ ۚ فَإِنِ اعْتَزَلُوكُمْ فَلَمْ يُقَاتِلُوكُمْ وَأَلْقَوْا إِلَيْكُمُ السَّلَمَ فَمَا جَعَلَ اللَّهُ لَكُمْ عَلَيْهِمْ سَبِيلًا ﴿٩٠﴾

91. Mtawakuta wengine wanaotaka kupata salama kwenu na kupata salama kwa watu wao; kila wakirudishwa katika fitina (na hao jamaa zao makafiri) huangushwa humo fitinani kifudifudi; (yaani huingia vyema katika fitina hiyo wakawataabisha Waislamu). Basi kama hawajitengi nanyi wala kukuleteeni amani wala kuzuia mikono yao, basi wakamateni na kuwaua po pote mnapowapata (kama wanavyokufanyieni). Na hao ndio ambao tumekupeni juu yao hoja zilizo dhahiri (za kujuzu kupigana nao).

سَتَجِدُونَ آخَرِينَ يُرِيدُونَ أَنْ يَأْمَنُوكُمْ وَيَأْمَنُوا قَوْمَهُمْ كُلَّمَا رُدُّوا إِلَى الْفِتْنَةِ أُرْكِسُوا فِيهَا ۚ فَإِنْ لَمْ يَعْتَزِلُوكُمْ وَيُلْقُوا إِلَيْكُمُ السَّلَمَ وَيَكُفُّوا أَيْدِيَهُمْ فَخُذُوهُمْ وَاقْتُلُوهُمْ حَيْثُ ثَقِفْتُمُوهُمْ ۚ وَأُولَٰئِكُمْ جَعَلْنَا لَكُمْ عَلَيْهِمْ سُلْطَانًا مُبِينًا ﴿٩١﴾ ع

92. Na haiwi kwa Muislamu kumwua Muislamu (mwenziwe kusudi) ila kwa kukosea. Na mwenye kumuua Muislamu kwa kukosea basi ampe

وَمَا كَانَ لِمُؤْمِنٍ أَنْ يَقْتُلَ مُؤْمِنًا إِلَّا خَطَأً ۚ وَمَنْ قَتَلَ مُؤْمِنًا خَطَأً فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ

---

wasingelimwacha Mtume na Waislamu wenziwao katika hali ile.

90. Katika vita vilivyokuwa vikitokea baina ya Mtume na Waarabu ilitokea kufanyiana suluhu na kuandikiana mikataba kuwa Mtume asipigane na kabila hiyo (wala asipigane na waitifaki wa kabila hiyo; japo hawana uitifaki na Mtume), wala kabila hiyo isipigane na Mtume wala wasipigane na waitifaki wa Mtume (japo kuwa si Waislamu).

Zilikuwa kabila nyingine waitifaki na Mtume wala hazikusilimu. Lakini hazimpigi Mtume wala Mtume hapigani nazo. Basi hizi Mtume ameambiwa asipigane nazo wala asipigane na waitifaki wao — japo waitifaki wao hao hawakufunga uitifaki na Mtume—lakini hawampigi Mtume pia.

Na zilikuwa kabila nyingine hazikufanya uitifaki na Mtume—kwa kuogopa wasiwaudhi jamaa zao—wala hawampigi Mtume japo jamaa zao wataingia vitani kumpiga Mtume. Basi na hawa nao Mtume kaambiwa asipigane nao maadamu hawana ugomvi na Waislamu.

91. Hapa inaamrishwa watiwe adabu barabara hao wanafiki ili waone ubaya wa ubaya wao huo, wapate kuuacha. Dawa ya moto ni moto.

92. Dhambi za kuua ni shadidi kabisa—ni kukaa milele tu Motoni kama ilivyotajwa katika Aya ya 93. Basi hii Aya ya 92 inasema kuwa haimkiniki kwa Mwislamu kusikia haya na akathubutu kumwua Mwislamu mwenzake; (bali na hata asiyekuwa Mwislamu kama alivyobainisha haya Mtume).

uungwana mtumwa (wake mmoja) aliye Muislamu; na .(pia) atoe diya (malipo) kuwapa warithi wake (huyo mtu aliyemwua). Isipokuwa waache wenyewe (hao warithi) kwa kufanya kuwa ni sadaka (yao). Na (aliyeuawa) akiwa ni jamaa wa maadui zenu, hali yeye ni Mwisilamu; basi ampe uungwana mtumwa aliye Mwislamu (basi; hapana wa kupewa diya). Na kama (aliyeuawa) ni mmoja wa watu ambao kuna ahadi baina yenu na baina yao; basi warithi wake wapewe malipo na pia apewe uungwana mtumwa aliye Mwislamu. Na asiyepata basi afunge miezi miwili inayofuatana. Ndiyo kitubio kitokacho kwa Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na) Mwenye hikima.

مُؤْمِنَةٍ وَدِيَةٌ مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ إِلَّا أَن
يَصَّدَّقُوا ۚ فَإِن كَانَ مِن قَوْمٍ عَدُوٍّ لَّكُمْ وَهُوَ
مُؤْمِنٌ فَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۖ وَإِن كَانَ
مِن قَوْمٍ بَيْنَكُمْ وَبَيْنَهُم مِّيثَاقٌ فَدِيَةٌ
مُّسَلَّمَةٌ إِلَىٰ أَهْلِهِ وَتَحْرِيرُ رَقَبَةٍ مُّؤْمِنَةٍ ۖ
فَمَن لَّمْ يَجِدْ فَصِيَامُ شَهْرَيْنِ مُتَتَابِعَيْنِ تَوْبَةً
مِّنَ اللَّهِ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿٩٢﴾

93. Na mwenye kumwua Mwislamu kwa kukusudia, basi malipo yake ni Jahannam, humo atakaa milele; na Mwenyezi Mungu amemghadhibikia na amemlani na amemwandalia adhabu kubwa.

وَمَن يَقْتُلْ مُؤْمِنًا مُّتَعَمِّدًا فَجَزَاؤُهُ جَهَنَّمُ
خَالِدًا فِيهَا وَغَضِبَ اللَّهُ عَلَيْهِ وَلَعَنَهُ وَأَعَدَّ لَهُ
عَذَابًا عَظِيمًا ﴿٩٣﴾

94. Enyi mlioamini! Mtakaposafiri katika njia ya Mwenyezi Mungu, basi msifanye jambo ila kwa ithibati, wala msimwambie yule anayekutoleeni salamu (ya kwamba): "Wewe si Mwislamu;

يَا أَيُّهَا الَّذِينَ آمَنُوا إِذَا ضَرَبْتُمْ
فِي سَبِيلِ اللَّهِ فَتَبَيَّنُوا وَلَا تَقُولُوا لِمَنْ أَلْقَىٰ

---

Lakini inamkini kwa kukosea kama vile (a) Anapiga kitu; silaha ile ikampata mtu ikamwua (b) Au kampiga kwa kitu kisichoua. Lakini kikamwua.

Basi ikiwa hivi—na kamwua Mwislamu mwenye jamaa walio Waislamu—basi itampasa mambo mawili—moja baina yake na Mwenyezi Mungu; na moja baina yake na hao aliowaulia mtu wao. Lililo baina yake na Mwenyezi Mungu ni (a) Kumpa uungwana (uhuru) mmoja katika watumwa wake. Au atanunua mtumwa ampe uhuru.

Na lililo baina yake na wale waliouliwa mtu wao ni (a) Kuwapa ngamia 100. Na katika nchi zisizotumia ngamia atoe thamani ya ngamia 100. Na kutoa huku kunaitwa Diya. Basi itampasa atoe diya hii.

Ila wenyewe hao waliouliwa mtu wao wakisamehe.

Na ikiwa yule aliyemwua ni Mwislamu—lakini jamaa zake ni makafiri wanaopigana na Waislamu—basi itampasa ile haki ya Mungu tu; ya kumfanya mtumwa huru; haitampasa kutoa diya.

Na akiwa huyo aliyemwua ni Mwislamu—na jamaa zake makafiri wasiopigana na Waislamu—basi yatampasa yote mawili (a) Ile haki ya Mungu na (b) Haki ya wale mawarithi; ya kuwapa diya.

Na ile haki ya Mungu ya kumpa mtumwa uungwana ikimshinda—kwa kuwa hana (a) mtumwa wala hana (b) pesa za kununulia au (c) hapana watumwa—basi atafunga miezi miwili mfululizo; asiache hata siku moja. Akiacha hata siku moja zitaharibika zote zile za nyuma. Aianze kuifunga tena upya hiyo miezi miwili.

93. Hapa inatajwa ikabu kubwa kabisa inayomngoja mwenye kuua, huko Akhera. Nayo ni moto wa Jahannam wa daima milele. Ulamaa wengine wanasema kuwa Mwenye kuua kusudi haikubaliwi toba yake hata akitubia vipi.

Na kama ilivyokuwa haramu kumwua mwenzio ndio vile vile haramu kujiua. Roho yako si yako, ukasema 'Nitaitoa nitakapotaka.' Roho ni Yake Mwenyewe Mwenyezi Mungu; amekupa hadiya, na hakukupa idhini kuitumia unavyotaka kuitumia.

Na ulamaa wengine wanasema kuwa "Mtu aliyejiua hapana ruhusa kusalia wala kuombewa dua. Aoshwe, akafiniwe, atiwe kaburini; uvundo wake ufunikike. Na udhia wishe, basi.

Kwa namna yo yote ile ya kujiua si kuzuri, kukiwa kwa mara moja, kama kujitia kitanzi, au kujiua kidogo kidogo. Huku kunasogelea katika kujiua kwa ghafla, kama kulewa kwa maspiriti, kuvuta bangi na kama haya.

94. Hapa wanakatazwa Waislamu kumdhani wasiyemjua kuwa ni adui yao, wakamwua tu kama wao (hao maadui) wanavyowaua Waislamu. Wanaambiwa wayakinishe kwanza barabara.

(mkamwua); mnataka mafao ya dunia hii, hali ya kuwa kwa Mwenyezi Mungu kuna ghanima nyingi kabisa. Bali hivi ndivyo mlivyokuwa zamani, Mwenyezi Mungu akakufanyieni ihsani (mkajua Uislamu mkasilimu). Basi chungueni sawa sawa. Hakika Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda.

إِلَيْكُمُ السَّلَٰمَ لَسْتَ مُؤْمِنًا ۚ تَبْتَغُونَ عَرَضَ
الْحَيَوٰةِ الدُّنْيَا فَعِنْدَ اللَّهِ مَغَانِمُ كَثِيرَةٌ ۚ كَذَٰلِكَ
كُنْتُمْ مِنْ قَبْلُ فَمَنَّ اللَّهُ عَلَيْكُمْ فَتَبَيَّنُوا ۚ إِنَّ
اللَّهَ كَانَ بِمَا تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿٩٤﴾

95. Hawawi sawa Waislamu wanaokaa wasende vitani, isipokuwa wenye dharura. (Hawawi sawa) na wale wapiganao katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na kwa nafsi zao. Mwenyezi Mungu amewafadhilisha katika cheo wale wapiganao katika njia ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na kwa nafsi zao kuliko wakaao (wasende kupigana). Ingawa Mwenyezi Mungu amewaahidi wote (kupata) wema, lakini Mwenyezi Mungu amewafadhilisha—wale wapiganao kuliko wakaao—kwa ujira mkuu

لَا يَسْتَوِي الْقَٰعِدُونَ مِنَ الْمُؤْمِنِينَ غَيْرُ أُولِي
الضَّرَرِ وَالْمُجَٰهِدُونَ فِي سَبِيلِ اللَّهِ بِأَمْوَٰلِهِمْ
وَأَنْفُسِهِمْ ۚ فَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَٰهِدِينَ بِأَمْوَٰلِهِمْ
وَأَنْفُسِهِمْ عَلَى الْقَٰعِدِينَ دَرَجَةً ۚ وَكُلًّا
وَعَدَ اللَّهُ الْحُسْنَىٰ ۚ وَفَضَّلَ اللَّهُ الْمُجَٰهِدِينَ عَلَى
الْقَٰعِدِينَ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿٩٥﴾

96. (Watapata) vyeo vikubwa vitokavyo kwake, na msamaha na rehema. Na Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

دَرَجَٰتٍ مِنْهُ وَمَغْفِرَةً وَرَحْمَةً ۚ وَكَانَ اللَّهُ
غَفُورًا رَحِيمًا ﴿٩٦﴾

97. Wale ambao Malaika wamewafisha, hali wamedhulumu nafsi zao, (kwa kutohajiri; Malaika) watawaambia: "Mlikuwa katika hali gani (katika jambo la dini yenu?)" Watasema: "Tulikuwa madhaifu katika ardhi hiyo (kwa hivyo hatukuweza kufanya ibada yetu." (Malaika) watasema: "Ardhi ya Mwenyezi Mungu haikuwa na wasaa na nyinyi, kuhamia humo?" Basi hao makazi yao ni Jahannam; nayo ni marejeo mabaya kabisa

إِنَّ الَّذِينَ تَوَفَّىٰهُمُ الْمَلَٰئِكَةُ ظَالِمِي أَنْفُسِهِمْ
قَالُوا فِيمَ كُنْتُمْ ۖ قَالُوا كُنَّا مُسْتَضْعَفِينَ فِي
الْأَرْضِ ۚ قَالُوا أَلَمْ تَكُنْ أَرْضُ اللَّهِ وَٰسِعَةً
فَتُهَاجِرُوا فِيهَا ۚ فَأُولَٰئِكَ مَأْوَىٰهُمْ جَهَنَّمُ ۖ
وَسَاءَتْ مَصِيرًا ﴿٩٧﴾

98. Isipokuwa wale waliokuwa madhaifu kweli; katika wanaume na wanawake na watoto wasio na uweza wa hila yo yote wala hawawezi kuongoza njia (kwenda Madina)

إِلَّا الْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ الرِّجَالِ وَالنِّسَاءِ وَ
الْوِلْدَٰنِ لَا يَسْتَطِيعُونَ حِيلَةً وَلَا يَهْتَدُونَ
سَبِيلًا ﴿٩٨﴾

99. Basi hao huenda Mwenyezi Mungu akawasamehe; Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kughufiria.

فَأُولَٰئِكَ عَسَى اللَّهُ أَنْ يَعْفُوَ عَنْهُمْ ۚ وَكَانَ اللَّهُ
عَفُوًّا غَفُورًا ﴿٩٩﴾

---

95. Hapa wanahimizwa watu kupigania dini kwa mali yao na kwa nafsi zao.

97.-99. Hapo zamani alipohama Mtume pamoja na Sahaba zake kwenda Madina alilazimishwa kila aliye Mwislamu asisalie katika mji wa ukafiri. Aache mali zake na watoto wake na kila chake ende huko Madina, kwani hapo katika mji wa kikafiri hataweza kufanya amali za dini yake. Uislamu wake utakuwa vipi—hauna amali! Uislamu ni Amali—si Itikadi tupu.

Basi ndio wanalaumiwa hapa na kuambiwa kuwa watakufa vibaya, ila wale ambao walikuwa hawana njia yo yote ya kuweza kuhama kwenda huko Madina.

Na hao pia wamo khatarini kwani; labda wanaonekana kwa dhahiri tu kuwa hawawezi, na ikitazamwa kweli itaonekana kuwa wanaweza, Basi na wao wamo khatarini pia.

Wengine hao waliosalia Makka walitolewa na makafiri kwenda katika vita vya Badri kumpiga Mtume; wakenda, na nia yao wasimpige Mwislamu. Lakini haukukubaliwa kwao huo kuwa udhuru.

100. Na mwenye kuhama kwa ajili ya dini ya Mwenyezi Mungu, atapata mahali pengi ardhini humu pa kukimbilia, na (atapata) wasaa. Na anayetoka katika nyumba yake ili kuhama kwa ajili ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake, kisha yakamfika mauti (njiani), basi umehakikika ujira wake juu ya Mwenyezi Mungu. Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

101. Na mnaposafiri katika ardhi, si vibaya kwenu kama mkifupisha Sala, iwapo mnaogopa ya kwamba wale waliokufuru watakutaabisheni. Bila shaka makafiri ni maadui zenu dhahiri.

102. Na unapokuwa pamoja nao (Waislamu katika vita) ukawasalisha; basi kundi moja miongoni mwao wasimame pamoja nawe (wanasali), na washike silaha zao. Na watakapomaliza sijida zao

وَمَن يُهَاجِرْ فِي سَبِيلِ اللَّهِ يَجِدْ فِي
الْأَرْضِ مُرَاغَمًا كَثِيرًا وَسَعَةً ۚ وَمَن يَخْرُجْ
مِن بَيْتِهِ مُهَاجِرًا إِلَى اللَّهِ وَرَسُولِهِ ثُمَّ
يُدْرِكْهُ الْمَوْتُ فَقَدْ وَقَعَ أَجْرُهُ عَلَى اللَّهِ ۗ
وَكَانَ اللَّهُ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٠٠﴾

وَإِذَا ضَرَبْتُمْ فِي الْأَرْضِ فَلَيْسَ عَلَيْكُمْ جُنَاحٌ أَن
تَقْصُرُوا مِنَ الصَّلَاةِ إِنْ خِفْتُمْ أَن يَفْتِنَكُمُ الَّذِينَ
كَفَرُوا ۚ إِنَّ الْكَافِرِينَ كَانُوا لَكُمْ عَدُوًّا مُّبِينًا ﴿١٠١﴾
وَإِذَا كُنتَ فِيهِمْ فَأَقَمْتَ لَهُمُ الصَّلَاةَ
فَلْتَقُمْ طَائِفَةٌ مِّنْهُمْ مَّعَكَ وَلْيَأْخُذُوا أَسْلِحَتَهُمْ

100. Wanahimizwa kuhama na kutiwa moyo kuwa huko wanakokwenda watafanikiwa.

Na wanahimizwa hata vizee na wagonjwa wahame. Na hata ikitokea bahati mbaya wakafa njiani—itahisabika kuwa walihama, wapate thawabu za kama hao waliohama wakaja wakakaa Madina na Mtume, wakapigania dini.

Na vile vile mtu akitoka kwenda kuhiji akafa wala hajamaliza amali za Hija—au kabla hajaifanya hata moja—atahisabika mbele ya Mwenyezi Mungu kuwa kahiji. Lakini na hapa atahijiwa.

101. Ilivyokuwa Waislamu wamehimizwa kuhajiri basi wamepunguziwa baadhi ya shida za njiani. Kama kusali. Wanapata ruhusa (a) Kuzipunguza sala za rakaa nne nne wazisali kwa rakaa mbili mbili. Na wanapata ruhusa (b) Kusali mara 3 badala ya mara 5. Sala ya Adhuhuri na Laasiri anaweza mtu kuzisali wakati mmoja. Ima wakati wa adhuhuri au wakati wa laasiri. Wakati huo huo atasali rakaa mbili za Adhuhuri, kisha asali rakaa mbili za Laasiri.

Na Sala ya Magharibi na ya Isha anaweza kuzisali wakati mmoja. Wakati huo huo atasali rakaa 3 za Magharibi, kisha asali rakaa mbili za Isha.

Sala ya Asubuhi tu ndiyo inayosaliwa kwa wakati wake ule ule wa daima.

Hukumu hii ilitolewa hapo Waislamu walipokuwa na khofu katika safari zao, kuogopa makafiri. Na baada ya kuondoka khofu hizo imeachiwa vivyo hivyo. Mpaka leo—zama za aeroplane na vipando vyengine vya raha—hukumu inakwenda ile ile ya kupata ruhusa (a) Kupunguza na (b) kuchanganya.

Na tazama makadiyani walivyopotoa maelezo ya Aya hii waliyoihisabu kuwa ni ya 102. Walisema maneno haya: "Maneno haya hayasemi kuwa rakaa za Sala zipunguzwe . . . .". Na hali ya kuwa ndivyo inavyofasiriwa na wanavyuoni wote ila hao wawili watatu, na hao hapana yakini kuwa wamesema hivyo, ila wananasibishiwa kuwa wamesema hivi. Utaona katika sahifa 119 ya juzuu ya 5 imeandikwa hivi: *"An Taqsuruu Baadhas Salati Bitansyfiha" (Kupunguzwa baadhi ya Sala kusaliwa kwa nusu ya rakaa zake yaani Adhuhuri, Laasiri na Isha).* Wao wanadai sivyo hivi. Na ndivyo ulimwengu mzima wa Kiislamu unavyosema. Na hiyo kauli waliyoitia nguvu wao utaona vitabu vyote vya tafsiri — kama *Ruuhul Maany* katika sahifa 121 ya hii Juuzu ya 5—vinasema: *"Waqaala Baadhuhum Innal Qasra Fil Ayati Mahmuulun Alaa Qasril Ahwaal Minal Iymai Watakhfifit Tasbyhi . . . Wanusiba ila Taawuus wadh Dhahhak."* (Wengine wanasema muradi wake kupunguza hali zake . . . na kwa kupunguza *Subhana* . . . Na Kauli hii inanasibishiwa *Taawus* na *Adh Dhahhak).* Na wao wameonyesha kuwa hii ndio kauli barabara.

Na Mwenyezi Mungu alizidi kuwahizi waliposema: "Tafsiri hii imetolewa na Ibn Kathir na kukubaliwa na Mujaahid na Adh Dhahhak". Wanataka kusema uwongo nao wajinga wa tarikhi. Wameandika kuwa Kauli hii kaitaja Ibni Kathir wakaikublai hao kina Mujahidi na Adh Dhahhak. Masikini! Wamehizika! Hawajui kuwa Ibni Kathir alikuwa katika karne ya nane (700), na kina Mujahid kwenye karne ya kwanza (100)! Vipi watu waliokuwa katika karne ya kwanza (100) watayaona maneno ya mtu aliyekuwa katika karne ya nane (700)? Hizaya daima itawafika kwa ajili ya uwongo wao. Akalikwakwara Kwakwa.

102. Sala ya Jamaa inahimizwa sana sana. Basi hata vitani huko ukifika wakati wa sala wanaambiwa wasali jamaa. Lakini hawasali wote wakati mmoja. Hugawiwa sehemu mbili. Sehemu moja hubaki imekabili maadui, na sehemu moja ikawa inasali na Imamu. Na sala zote huko husaliwa rakaa mbili mbili ila Magharibi.

basi nawende nyuma yenu (kwa kulinda); na lije kundi jingine ambalo halijasali, lisali pamoja nawe, nao washike hadhari yao na silaha zao (humo ndani ya Sala; maana) wale waliokufuru wanataka mghafilike na silaha zenu na vitu vyenu ili wakuvamieni mvamio wa mara moja. Wala si vibaya kwenu ikiwa mnaona udhia kwa sababu ya mvua au mnao ugonjwa, kuondoa silaha zenu. Na mshike hadhari yenu. Hakika . Mwenyezi Mungu amewaandalia makafiri adhabu itakayowadhalilisha.

فَإِذَا سَجَدُوا فَلْيَكُونُوا مِن وَرَائِكُمْ وَلْتَأْتِ
طَائِفَةٌ أُخْرَىٰ لَمْ يُصَلُّوا فَلْيُصَلُّوا مَعَكَ
وَلْيَأْخُذُوا حِذْرَهُمْ وَأَسْلِحَتَهُمْ ۗ وَدَّ الَّذِينَ
كَفَرُوا لَوْ تَغْفُلُونَ عَنْ أَسْلِحَتِكُمْ وَأَمْتِعَتِكُمْ
فَيَمِيلُونَ عَلَيْكُم مَّيْلَةً وَاحِدَةً ۚ وَلَا جُنَاحَ
عَلَيْكُمْ إِن كَانَ بِكُمْ أَذًى مِّن مَّطَرٍ أَوْ كُنتُم
مَّرْضَىٰ أَن تَضَعُوا أَسْلِحَتَكُمْ ۖ وَخُذُوا حِذْرَكُمْ ۗ
إِنَّ اللَّهَ أَعَدَّ لِلْكَافِرِينَ عَذَابًا مُّهِينًا ﴿١٠٢﴾

103. Mwishapo kusali kuweni mnamkumbuka Mwenyezi Mungu (vile vile)—msimamapo na mkaapo na (mlalapo) ubavu. Na mtakapopata amani (mkawa katika salama, hapana vita), basi simamisheni Sala (kama dasturi). Kwa hakika Sala kwa Waislamu ni faradhi iliyowekewa nyakati makhsusi.

فَإِذَا قَضَيْتُمُ الصَّلَاةَ فَاذْكُرُوا اللَّهَ قِيَامًا وَ
قُعُودًا وَعَلَىٰ جُنُوبِكُمْ ۚ فَإِذَا اطْمَأْنَنتُمْ فَأَقِيمُوا
الصَّلَاةَ ۚ إِنَّ الصَّلَاةَ كَانَتْ عَلَى الْمُؤْمِنِينَ
كِتَابًا مَّوْقُوتًا ﴿١٠٣﴾

104. Wala msifanye uvivu kuwafuatia watu (walio maadui). Kama mmepata maumivu basi wao pia wanapata maumivu kama mnavyoumia. Na nyinyi mnatumai kwa Mwenyezi Mungu wasiyoyatumai. Na Mwenyezi Mungu ndiye Mjuzi na Mwenye hikima.

وَلَا تَهِنُوا فِي ابْتِغَاءِ الْقَوْمِ ۖ إِن تَكُونُوا تَأْلَمُونَ
فَإِنَّهُمْ يَأْلَمُونَ كَمَا تَأْلَمُونَ ۖ وَتَرْجُونَ مِنَ اللَّهِ
مَا لَا يَرْجُونَ ۗ وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١٠٤﴾ ع

105. Hakika tumekuteremshia Kitabu (hiki), hali ya kuwa kimeshikamana na haki ili upate kuhukumu baina ya watu kama alivyokufahamisha Mwenyezi

إِنَّا أَنزَلْنَا إِلَيْكَ الْكِتَابَ بِالْحَقِّ لِتَحْكُمَ بَيْنَ

---

Basi Imamu atasali rakaa moja na hawa anaosali nao. Watakaponyanyuka kusali rakaa ya pili, kila mtu atamaliza rakaa yake ile peke yake upesi upesi, akae asome Tahiyyatu atoe salamu. Imamu atasimama tu anaendelea tu kusoma—ikisha Sura hii anaanza hii. Mpaka wale waliotoa salamu wende kule waliko wenzao wakabiliane wao na maadui sasa, na wale waliokuwa wamekabiliana na maadui waje wamfuate Imamu.

Imamu akihisi kishafuatwa na wote, atarukuu pamoja nao. Awe kawasalisha rakaa moja ile. Ikimalizika, yeye atakaa kusoma Tahiyyatu—awangojee hapo katika kitako cha Tahiyyatu, asitoe salamu. Na wale watanyanyuka kuimaliza ile rakaa yao moja iliyosalia. Wakifika katika Tahiyyatu watakaa kuisoma. Imamu akihisi kuwa wote wamekwishakaa wanamaliza Tahiyyatu atatoa salamu; na wao watoe.

Hii ni namna moja katika namna inavyosaliwa Sala ya Jamaa katika vita.

Na wanaposali husali na Silaha zao kamili—wamejitatiza mishare, wamejifunga majambia, wamevaa kofia za chuma, wamekamata mikuki au panga. (Na zama za sasa bunduki, bastola na vyenginevyo. Kila zama na Silaha zake na mambo yake). Ila pakiwa na udhuru—kama hizo zilizotajwa mwisho wa Aya hii—basi atapata ruhusa kupunguza hizo Silaha zake au kuziacha kabisa.

103. Inatakikana kwa Mwislamu kila wakati kuwa anamkumbuka Mwenyezi Mungu—si ndani ya Sala tu. Katika kila hali zake awe anamkumbuka Mwenyezi Mungu, na maamrisho yake ili ayafanye na makatazo yake ili ajiepushe nayo.

104. Wanahimizwa Waislamu kuipigania dini hata wakipata taabu namna gani na maumivu yaliyoje, kwani wanalolipigania ni kubwa kabisa mno. Hapana kikubwa kinachopatikana bure. Mtaka cha mvunguni huinama, seuze vya mbinguni.

106.-107. Anatakiwa Mtume — na sisi sote ndiyo kabisa — asiwe mwenye kupendelea. Aone watu wote

Mungu; wala usiwe mwenye kuwatetea wale wafanyao khiyana

النَّاسِ بِمَا أَرَىٰكَ اللَّهُ ۚ وَلَا تَكُن لِّلْخَائِنِينَ
خَصِيمًا ﴿١٠٥﴾

106. Na mwombe Mwenyezi Mungu maghufira. Bila shaka Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa kusamehe (na) Mwingi wa kurehemu.

وَاسْتَغْفِرِ اللَّهَ ۖ إِنَّ اللَّهَ كَانَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١٠٦﴾

107. Wala usiwatetee wale wanaokhini nafsi zao. Hakika Mwenyezi Mungu hampendi aliye khaini mwenye dhambi

وَلَا تُجَادِلْ عَنِ الَّذِينَ يَخْتَانُونَ أَنفُسَهُمْ ۚ إِنَّ
اللَّهَ لَا يُحِبُّ مَن كَانَ خَوَّانًا أَثِيمًا ﴿١٠٧﴾

108. Wanastahi watu lakini hawamstahi Mwenyezi Mungu; naye alikuwa yu pamoja nao; (nao hawana habari) pale waliposhauriana kwa zile kauli asizozipenda. Na Mwenyezi Mungu anayajua vyema yote wanayoyatenda.

يَسْتَخْفُونَ مِنَ النَّاسِ وَلَا يَسْتَخْفُونَ مِنَ اللَّهِ
وَهُوَ مَعَهُمْ إِذْ يُبَيِّتُونَ مَا لَا يَرْضَىٰ مِنَ
الْقَوْلِ ۚ وَكَانَ اللَّهُ بِمَا يَعْمَلُونَ مُحِيطًا ﴿١٠٨﴾

109. Angalieni. Nyinyi mmewatetea katika maisha ya dunia (hapa ulimwenguni) Lakini ni nani atakayemjadili Mwenyezi Mungu siku ya Kiyama kwa ajili yao, au ni nani atakayekuwa mlinzi juu yao?

هَا أَنتُمْ هَٰؤُلَاءِ جَادَلْتُمْ عَنْهُمْ فِي الْحَيَاةِ
الدُّنْيَا فَمَن يُجَادِلُ اللَّهَ عَنْهُمْ يَوْمَ الْقِيَامَةِ
أَم مَّن يَكُونُ عَلَيْهِمْ وَكِيلًا ﴿١٠٩﴾

110. Na mwenye kutenda uovu (wa kuwachukiza wenziwe) au akajidhulumu nafsi yake (kwa kufanya kosa la kumdhuru mwenyewe tu); kisha akaomba maghufira kwa Mwenyezi Mungu, atamkuta Mwenyezi Mungu ni Mwenye kughufiria (na) Mwenye kurehemu. (Lakini naawatake msamaha hao aliowakosa pia mpaka waridhike).

وَمَن يَعْمَلْ سُوءًا أَوْ يَظْلِمْ نَفْسَهُ ثُمَّ يَسْتَغْفِرِ
اللَّهَ يَجِدِ اللَّهَ غَفُورًا رَّحِيمًا ﴿١١٠﴾

111. Na mwenye kufanya dhambi, basi ameifanyia nafsi yake (uovu). Na Mwenyezi Mungu ndiye Ajuaye (na) ndiye Mwenye hikima.

وَمَن يَكْسِبْ إِثْمًا فَإِنَّمَا يَكْسِبُهُ عَلَىٰ نَفْسِهِ ۚ
وَكَانَ اللَّهُ عَلِيمًا حَكِيمًا ﴿١١١﴾

---

kwake sawa sawa. Asivutike kwa uhodari wa kusema wa baadhi ya wanaoshitakiana. Na awe na hadhari, na kutaka msamaha kila wakati isiwe kapata kuvutika bila ya mwenyewe kutambua.

108. Watu utaona wanajificha wanapofanya mambo yao ili watu wasiwaone. Lakini hawabali kuonekana na Mwenyezi Mungu: naye ndiye atakayewalipa. Na kila wakati na katika kila hali Mwenyezi Mungu yu pamoja nao — anajua yote yanayopita katika nyoyo zao, na anayasikia yote wanayoyasema na anayaona yote wanayoyatenda. Wa kuogopwa kweli kweli ni Mungu kwani ndiye anayeweza kufanya atakalo.

109. Hapa wanakatazwa watu kuwapigania watu wabaya. Waache walipwe kwa mabaya yao ili wapewe nyoyo kidogo wale wanaowafanyia mabaya hayo. Basi nawatahadhari mawakili kuwapigania watu ambao wana yakini kuwa wao ndio madhalimu wenye kuonea watu — sio wenye kuonewa. Nawatahadhari mawakili kuwasimamia watu hao; hata wakiwapa nini. Nawawasimamie wale wenye kuonewa; hapo watapata huo ujira walioahidiwa na watapata thawabu za Mwenyezi Mungu kwa kupigania haki. Mawakili wakishika njia hii watafuzu duniani na Akhera.

110. Anawahimiza Mwenyezi Mungu maasi warejee upesi kwake kwa (a) Kuacha hayo wanayofanya na (b) Kuazimia barabara kutofanya tena kattu na (c) Kujuta kwa yaliyopita na (d) Kuwarejeshea wenyewe haki zao hao aliowadhulumu au (e) Kuwataka radhi na msamaha. Wakifanya hivi papo hapo Mwenyezi Mungu atawapokea Inshaallah.

111. Wanabainishiwa kuwa mwovu anajidhulumu mwenyewe; asione tamu kuwa anadhulumu wenziwe; anajidhulumu mwenyewe hivyo kwani Mwenyezi Mungu atamlipa tu, ima Akhera au papa hapa duniani. 'Mla cha mwenziwe na chake huliwa' na 'Mosha hoshwa' (Mwosha huoshwa).

112. Na mwenye kufanya khatia (ndogo) au dhambi (kubwa), kisha akamsingizia (nayo) asiye na kosa, basi kwa yakini amebeba dhulma kubwa na dhambi zilizo dhahiri.

وَمَن يَكْسِبْ خَطِيٓـَٔةً أَوْ إِثْمًا ثُمَّ يَرْمِ بِهِۦ بَرِيٓـًٔا فَقَدِ
ٱحْتَمَلَ بُهْتَـٰنًا وَإِثْمًا مُّبِينًا ﴿١١٢﴾

113. Na kama si kuwa ziko juu yako fadhila za Mwenyezi Mungu na rehema Zake, bila shaka kundi moja katika hao wangalikusudia kukupoteza. Na hao wasingezipoteza ila nafsi zao. Wala hawataweza kukudhuru cho chote. Na Mwenyezi Mungu amekuteremshia Kitabu na hikima na amekufundisha uliyokuwa huyajui. Na fadhila za Mwenyezi Mungu zilizo juu yako ni kubwa (kabisa).

وَلَوْلَا فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكَ وَرَحْمَتُهُۥ لَهَمَّت
طَّآئِفَةٌ مِّنْهُمْ أَن يُضِلُّوكَ وَمَا يُضِلُّونَ إِلَّآ
أَنفُسَهُمْ وَمَا يَضُرُّونَكَ مِن شَىْءٍ وَأَنزَلَ ٱللَّهُ
عَلَيْكَ ٱلْكِتَـٰبَ وَٱلْحِكْمَةَ وَعَلَّمَكَ مَا لَمْ تَكُن
تَعْلَمُ وَكَانَ فَضْلُ ٱللَّهِ عَلَيْكَ عَظِيمًا ﴿١١٣﴾

114. Hakuna kheri katika mengi wanayoshauriana kwa siri. Isipokuwa (mashauri ya) wale wanaoamrisha kutoa sadaka au kufanya mema au kupatanisha baina ya watu. Na atakayefanya hivi kwa kutaka radhi ya Mwenyezi Mungu, basi tutampa ujira mkubwa.

لَّا خَيْرَ فِى كَثِيرٍ مِّن نَّجْوَىٰهُمْ إِلَّا مَنْ أَمَرَ
بِصَدَقَةٍ أَوْ مَعْرُوفٍ أَوْ إِصْلَـٰحٍۭ بَيْنَ ٱلنَّاسِ
وَمَن يَفْعَلْ ذَٰلِكَ ٱبْتِغَآءَ مَرْضَاتِ ٱللَّهِ فَسَوْفَ
نُؤْتِيهِ أَجْرًا عَظِيمًا ﴿١١٤﴾

115. Na atakayemwasi Mtume baada ya kumdhihirikia uwongofu na akafuata njia isiyokuwa ya Waislamu, tutamgeuza alikogeukia mwenyewe na tutamwingiza katika Jahannam; napo ni pahali pabaya kabisa pa mtu kurudia.

وَمَن يُشَاقِقِ ٱلرَّسُولَ مِنۢ بَعْدِ مَا تَبَيَّنَ لَهُ
ٱلْهُدَىٰ وَيَتَّبِعْ غَيْرَ سَبِيلِ ٱلْمُؤْمِنِينَ نُوَلِّهِۦ
مَا تَوَلَّىٰ وَنُصْلِهِۦ جَهَنَّمَ وَسَآءَتْ مَصِيرًا ﴿١١٥﴾

116. Hakika Mwenyezi Mungu hasamehi (dhambi ya) kushirikishwa na kitu, (kukifanya ni mungu nacho ukakiabudu, ukakiomba . . .). Lakini yeye husamehe yasiyokuwa hayo kwa amtakaye. Na anayemshirikisha Mwenyezi Mungu, basi bila shaka yeye amekwishapotea upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).

إِنَّ ٱللَّهَ لَا يَغْفِرُ أَن يُشْرَكَ بِهِۦ وَيَغْفِرُ مَا دُونَ
ذَٰلِكَ لِمَن يَشَآءُ وَمَن يُشْرِكْ بِٱللَّهِ فَقَدْ ضَلَّ
ضَلَـٰلًۢا بَعِيدًا ﴿١١٦﴾

---

112. Na kuna watu wanaofanya mambo wao; kisha akamsingizia mwenziwe, jukumu la hayo likamwangukie yeye. Atakiona siku ya Kiama, au papa hapa duniani, kilichomtoa Kanga Manyoya.

113. Hapa Mwenyezi Mungu anataja kuwa hakuna fadhila mtu aliyopewa na Mwenyezi Mungu iliyo kubwa zaidi—baada ya kuumbwa na kupewa Uislamu—kuliko fadhila ya kupewa Ilimu. Kila mema ya duniani na Akhera yanapatikana kwa Ilimu. Qurani yote na Hadithi za Mtume zinahimiza kweli kweli kutafuta Ilimu—ya kutengeneza Akhera na ya kutengeneza dunia pia. Na hii Qurani na hizi Hadithi za Mtume zinahimiza hata kutoka NJE MBALI kabisa kutafuta hiyo Ilimu. Baadhi ya hizi Aya za Qurani zilizohimiza haya ni Aya ya 122 ya *Suratut Tawba.*

114. Hapa yanatajwa mazungumzo yaliyo mazuri watu kuzungumza. Ni mazungumzo ya kuamrisha mema na kukataza mabaya na kupatanisha; na yaliyo kama haya.

115. Aya hii ni kali kabisa vile vile kwa wale wanaoshikamana na mabidaa, wakaacha aliyokuja nayo Mtume, hata wakiambiwa kuwa hayo yanakhalifu aliyokuja nayo Mtume; kama haya Matahalili, Maarubaini, Mahauli na Kuyajangea makaburi misikiti (likawa kaburi ndani ya msikiti) na kuyajengea maziara na Kuyawashia taa na Kuyaomba, na kama haya. Na haya yote yamekatazwa kwa Hadithi za Mtume sahihi. Basi khiari zao. Nawazingatie vizuri Aya hii na nyinginezo chungu nzima, kama Aya ya 46 ya *Suratun Nisaa* na Aya ya 36 ya *Suratul Ahzab.*

117. Hawaabudu baada ya kumwacha Mwenyezi Mungu ila waungu wanawake; wala hawamwabudu (hakika) ila Shetani asi (kwani ndiye anayewazainishia hayo).

إِن يَدْعُونَ مِن دُونِهِۦٓ إِلَّآ إِنَٰثًا وَإِن يَدْعُونَ
إِلَّا شَيْطَٰنًا مَّرِيدًا ﴿١١٧﴾

118. (Ambaye) Mwenyezi Mungu amemlani. Naye (Shetani) alisema: (kumwambia Mwenyezi Mungu). "Kwa yakini nitashika sehemu maalumu katika waja wako"

لَّعَنَهُ ٱللَّهُ وَقَالَ لَأَتَّخِذَنَّ مِنْ عِبَادِكَ نَصِيبًا
مَّفْرُوضًا ﴿١١٨﴾

119. "Na nitawapoteza na nitawatumainisha na nitawaamrisha (ninavyotaka mimi). Basi watakata masikio ya wanyama (wawafanye kuwa hao ni wanyama watukufu); na nitawaamuru (pia. Nao) watabadili dini (yako) Mwenyezi Mungu." (Basi Mwenyezi Mungu anasema). "Na mwenye kumfanya shetani kuwa ni mlinzi (mungu wake) badala ya Mwenyezi Mungu, basi yeye amekhasiri khasara iliyo dhahiri."

وَلَأُضِلَّنَّهُمْ وَلَأُمَنِّيَنَّهُمْ وَلَءَامُرَنَّهُمْ فَلَيُبَتِّكُنَّ
ءَاذَانَ ٱلْأَنْعَٰمِ وَلَءَامُرَنَّهُمْ فَلَيُغَيِّرُنَّ خَلْقَ ٱللَّهِ
وَمَن يَتَّخِذِ ٱلشَّيْطَٰنَ وَلِيًّا مِّن دُونِ ٱللَّهِ فَقَدْ
خَسِرَ خُسْرَانًا مُّبِينًا ﴿١١٩﴾

120. (Shetani) anawaahidi (mambo ambayo hayatakuwa), na anawatumainisha (ambayo hawatayapata); kwani Shetani hawaahidi ila udanganyifu tu.

يَعِدُهُمْ وَيُمَنِّيهِمْ وَمَا يَعِدُهُمُ ٱلشَّيْطَٰنُ
إِلَّا غُرُورًا ﴿١٢٠﴾

---

117. Waarabu walikuwa wakiwaabudu Malaika na wakiwaitakidi kuwa ni watoto wanawake wa Mwenyezi Mungu. Na wao walikuwa wakiwaua watoto wao wanawake na wakiwadharau wanawake. Na huku wanaabudu miungu waliyoifanya kwa sura za wanawake. Ajabu kabisa. Wanawake wanawadharau na huku wanawafanya waungu wao kwa sura za kike.

Na hao waliopotea wakaabudu Malaika au jua au moto au vyenginevyo, katika hakika khasa hawamwabudu ila Shetani (Iblisi). Kwani Shetani ndiye anayewazainishia hayo.

118. Iblisi alipokuwa anatolewa mbinguni kishalaanika, alimwambia Mwenyezi Mungu kuwa atawazainishia maasi viumbe Vyake. Mwenyezi Mungu alimwambia kuwa hana nguvu ya kuweza kuwapoteza kwa nguvu; wakitaka wasitake. Watakaomfuata watakuwa wanamfuata kwa kutaka wenyewe, sio kwa kuwa wameshindwa nguvu kabisa kabisa, hawawezi kushindana naye. Siyo Watamfuata kwa kuwa anaweza kuwalazimisha wakitaka wasitake.

119. Yanatajwa baadhi ya mambo atakayowapotezea. Kuwatumainisha kuwa (a) Mwenyezi Mungu Ghafur Rahim; kuwa (b) Ukifanya kitu fulani au Ukisoma dua fulani utafutiwa dhambi zako zote, isisalie hata moja hata haki za watu; zote zitaruka pia; kuwa (c) Mabwana fulani na mabwana fulani watawaombea kila wanaojinasibisha nao katika mambo yao waliyowawekea; kuwa (d) Mabwana na mabibi fulani watawatia Peponi kila wanaotokana na kizazi chao; kuwa (e) Mtume hataridhia kumwona hata mtu mmoja katika umma wake yuko Motoni; kuwa (f) Maadamu mtu ni Mwislamu basi hatagusa Moto wa Jahannamu. Na huambia Manasara kuwa maadamu mtu Mnasara basi hatagusa Moto. Na huwaendea Mayahudi akawaambia vivi hivi. Na Mabaniani, Maparisi, Mabuda na wengineo wenye dini fulani au madhehebu mbali mbali akawadanganya kuwa maadamu wao wanafuata tarika fulani au madhehebu fulani au dini fulani basi Pepo inawangoja tu; bila msukosuko wo wote.

Na haya na kama hayo, ndiyo aliyoyavunja Mwenyezi Mungu katika Aya ya 123 ya *Suratin Nisaa* na mahala pengine.

| | |
|---|---|
| Thamani ya Pepo ukiitaka | Dhiki moyo wako kutozunguka |
| Thubutisha taa yake Rabuka | Mola akujazi majaza mema |
| Janati Naimu fil Janani | Jina na Insi waitamani |
| Jumla ya watu hawaioni | Ila kwa ambao watenda zema |
| Sharia husema: aso thawabu | Shida na mashaka yatamsibu |
| Shufaa ya Tumwal mahbubu | Huwa mbali naye na kumwegema. |

121. Hao mahali pao ni Jahannamu wala hawatapata makimbilio ya kutoka humo.

أُولَٰٓئِكَ مَأْوٰىهُمْ جَهَنَّمُ وَلَا يَجِدُونَ عَنْهَا
مَحِيصًا ﴿١٢١﴾

122. Na wale walioamini na kufanya vitendo vizuri, tutawaingiza katika Mabustani yapitayo mito mbele yake, watakaa humo milele. Ndiyo ahadi ya Mwenyezi Mungu iliyo kweli. Na nani mkweli zaidi kwa usemi kuliko Mwenyezi Mungu?

وَالَّذِينَ اٰمَنُوا وَعَمِلُوا الصّٰلِحٰتِ سَنُدْخِلُهُمْ جَنّٰتٍ
تَجْرِي مِنْ تَحْتِهَا الْاَنْهٰرُ خٰلِدِينَ فِيهَآ اَبَدًا ۚ
وَعْدَ اللّٰهِ حَقًّا ۚ وَمَنْ اَصْدَقُ مِنَ اللّٰهِ قِيلًا ﴿١٢٢﴾

123. (Kuingia Peponi) si kwa matamanio yenu, wala si kwa matamanio ya watu waliopewa Kitabu (kabla yenu. Lakini mambo ni haya): Atakayefanya ubaya atalipwa kwa (ubaya) huo wala hatapata mlinzi wala msaidizi kwa ajili yake mbele ya Mwenyezi Mungu.

لَيْسَ بِاَمَانِيِّكُمْ وَلَآ اَمَانِيِّ اَهْلِ الْكِتٰبِ ۚ مَنْ
يَعْمَلْ سُوٓءًا يُّجْزَ بِهٖ ۙ وَلَا يَجِدْ لَهٗ مِنْ دُونِ اللّٰهِ
وَلِيًّا وَّلَا نَصِيرًا ﴿١٢٣﴾

124. Na watakaofanya vitendo vizuri, wakiwa wanaume au wanawake, hali wao ni wenye kuamini, basi hao wataingia Peponi wala hawatadhulumiwa hata tundu ya kokwa ya tende.

وَمَنْ يَّعْمَلْ مِنَ الصّٰلِحٰتِ مِنْ ذَكَرٍ اَوْ اُنْثٰى
وَهُوَ مُؤْمِنٌ فَاُولٰٓئِكَ يَدْخُلُونَ الْجَنَّةَ
وَلَا يُظْلَمُونَ نَقِيرًا ﴿١٢٤﴾

125. Na nani aliye bora kwa dini kuliko yule ambaye ameuelekeza uso wake kwa Mwenyezi Mungu, naye ni mwema, na anafuata mila ya Ibrahimu (kuwa Mwislamu kweli kweli). Na Mwenyezi Mungu amemfanya Ibrahimu kuwa ni kipenzi chake.

وَمَنْ اَحْسَنُ دِينًا مِّمَّنْ اَسْلَمَ وَجْهَهٗ لِلّٰهِ وَ
هُوَ مُحْسِنٌ وَّاتَّبَعَ مِلَّةَ اِبْرٰهِيمَ حَنِيفًا ۗ
وَاتَّخَذَ اللّٰهُ اِبْرٰهِيمَ خَلِيلًا ﴿١٢٥﴾

126. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na Mwenyezi Mungu ndiye aliyevizunguka vitu vyote (kwa kuvijua nje yake na ndani yake).

وَلِلّٰهِ مَا فِي السَّمٰوٰتِ وَمَا فِي الْاَرْضِ ۚ وَكَانَ
اللّٰهُ بِكُلِّ شَيْءٍ مُّحِيطًا ﴿١٢٦﴾

127. Na wanakuuliza yanayowakhusu wanawake. Sema: "Mwenyezi Mungu anakwambieni khabari za hayo (sasa hivi). Na (pia yanakutajieni khabari hii) yale msomewayo katika Kitabu hiki juu ya wanawake mayatima ambao hamuwapi (mahari yao) waliyoandikiwa, na mnapenda kuwaoa. Na (yanakutajieni khabari hizi yale msomewayo katika Aya ya 2 na 12 ya Sura hii) juu ya walio dhaifu katika watoto. Na (anakwambieni) ya kwamba jitahidini kuwasimamia mayatima kwa insafu. Na wema wo wote mnaofanya Mwenyezi Mungu anajua. (Na ubaya vile vile).

وَيَسْتَفْتُونَكَ فِي النِّسَآءِ ۚ قُلِ اللّٰهُ يُفْتِيكُمْ
فِيهِنَّ ۙ وَمَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فِي الْكِتٰبِ فِي يَتٰمَى
النِّسَآءِ الّٰتِي لَا تُؤْتُونَهُنَّ مَا كُتِبَ لَهُنَّ وَ
تَرْغَبُونَ اَنْ تَنْكِحُوهُنَّ وَالْمُسْتَضْعَفِينَ مِنَ
الْوِلْدَانِ ۙ وَاَنْ تَقُومُوا لِلْيَتٰمٰى بِالْقِسْطِ ۚ وَمَا
تَفْعَلُوا مِنْ خَيْرٍ فَاِنَّ اللّٰهَ كَانَ بِهٖ عَلِيمًا ﴿١٢٧﴾

---

123. Wanakatazwa hapa watu kujidanganya roho zao, wakajinasibishia kupata wasiyoyastahiki ila kwa matamanio tu ya nafsi zao. "Wakiona vinaelea (vinaolea) vimeundwa," sio vimepatikana kwa matamanio. Kama kusema "Mimi wa Madhehebu fulani au wa Tarika fulani au wa Ukoo fulani basi nitapata . . ." Mizani ya kupata na kukosa imo katika Aya hii ya 124 na 125 na chungu nyinginezo zilizo kama hizi zilizojaa ndani ya Qurani yote nzima. Basi kipimo ni hicho cha kujulia kupata na kukosa.

127. Aya hii inahadidisha adhabu ya wenye kuwadhulumu wanawake, kama ilivyoshadidishwa adhabu ya wenye kuwadhulumu mayatima. Hao wote takriban ni wanyonge, basi isiwe "Mnyonge Msonge".

وَإِنِ امْرَأَةٌ خَافَتْ مِنْ بَعْلِهَا نُشُوزًا أَوْ
إِعْرَاضًا فَلَا جُنَاحَ عَلَيْهِمَا أَنْ يُصْلِحَا بَيْنَهُمَا
صُلْحًا ۚ وَالصُّلْحُ خَيْرٌ ۗ وَأُحْضِرَتِ الْأَنْفُسُ
الشُّحَّ ۚ وَإِنْ تُحْسِنُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ كَانَ بِمَا
تَعْمَلُونَ خَبِيرًا ﴿١٢٨﴾

128. Na kama mke akiona kwa mume wake kugombanagombana na kutenganatengana, basi si vibaya kwao wakitengeneza baina yao sulhu (njema wakastahmiliana vivyo hivyo bila kuachana); maana sulhu ni kitu bora. Na nafsi zimewekewa ubakhili mbele (ya macho yake). Na kama mkifanya mema (kuwafanyia wake zenu hao msiowapenda) na mkimcha Mwenyezi Mungu (msiwapunguzie haki zao, basi bila shaka Mwenyezi Mungu atakulipeni), kwani Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda.

وَلَنْ تَسْتَطِيعُوا أَنْ تَعْدِلُوا بَيْنَ النِّسَاءِ وَلَوْ حَرَصْتُمْ
فَلَا تَمِيلُوا كُلَّ الْمَيْلِ فَتَذَرُوهَا كَالْمُعَلَّقَةِ ۚ
وَإِنْ تُصْلِحُوا وَتَتَّقُوا فَإِنَّ اللَّهَ
كَانَ غَفُورًا رَحِيمًا ﴿١٢٩﴾

129. Nanyi hamwezi kufanya uadilifu (kweli-kweli) baina ya wake, ijapokuwa mtataka kufanya hivyo. Kwa hivyo msielekee (upande mmoja) kabisa kabisa; msije kumwacha (huyo mwengine msiyempenda) kama aliyeangikwa (aliyetundikwa anasukumika huku na huku; hajijui kuwa ana mume au mjane) Na mkisuluhiana (sasa) na mkamcha Mungu, basi Mwenyezi Mungu ni Mwingi wa msamaha (na) Mwingi wa rehema.

وَإِنْ يَتَفَرَّقَا يُغْنِ اللَّهُ كُلًّا مِنْ سَعَتِهِ ۚ وَكَانَ
اللَّهُ وَاسِعًا حَكِيمًا ﴿١٣٠﴾

130. Na kama wakitengana (kwa kuachana) Mwenyezi Mungu atamkwasisha kila mmoja katika wao kwa wasaa wake. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye wasaa (mkubwa kabisa) (na) Mwenye hikima.

وَلِلَّهِ مَا فِي السَّمَاوَاتِ وَمَا فِي الْأَرْضِ ۗ وَلَقَدْ
وَصَّيْنَا الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ مِنْ قَبْلِكُمْ وَإِيَّاكُمْ
أَنِ اتَّقُوا اللَّهَ ۚ وَإِنْ تَكْفُرُوا فَإِنَّ لِلَّهِ مَا فِي

131. Na ni vya Mwenyezi Mungu tu vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini. Na kwa yakini tuliwausia waliopewa Kitabu kabla yenu, na nyinyi (pia), kwamba mumche Mwenyezi Mungu. Na kama mkikataa basi (hamumdhuru Mwenyezi Mungu kitu, kwani) ni vya Mwenyezi Mungu tu

---

128. Mambo ya kuachana yanavunjwa nguvu sana katika Sharia ya Kiislamu. Na watu wengine mara huchokana wakaona taabu kutekelezeana haki zao za ndoa. Ima Mke hamkamilishii Mume haki zake au Mume hamkamilishii Mke haki zake.

Basi inataka yule asiyekamilishiwa asipande mori akaacha (akiwa mwanamume) au akataka kuachwa akiwa mwanamke. Kwani Subira yavuta Kheri.

Lakini nyoyo zina ubakhili. Kila mmoja hakubali kusamehe haki yake. Basi kila mtu apigane na moyo wake, akubali kusamehe baadhi ya haki zake—bali hata zote pia. Na Mwenyezi Mungu atampa thawabu kubwa.

Na wanawake ndiyo sana wasiokubali kuona wanaonewa. Basi ndiyo maana hapa akatajwa mke kuambiwa astahmili. Basi na mume ndiyo vivyo hivyo.

129. Tumebainisha katika maelezo ya Aya ya 3 ya hii *Suratin Nisaa* kuwa ukewenza umevunjwa nguvu sana na Uislamu; ila ikiwa hapana budi ndio ufanywe. Kwani moyo ni moyo. Takriba muhali moyo kupenda vitu viwili sawa sawa na kuvifanyia insafu sawa sawa. Lazima utamili kumoja.

Basi hapa wanaambiwa hao waume wenye kuweka ukewenza kuwa wakimili upande mmoja wajitahidi mwisho wa jitihada yao wasimili kabisa kabisa, hata akawa huyo mwengine hajijui kuwa mke au si mke. Anajiona katundikika kwa uzi; anasukumika huku na huku; hajijui kasimama wapi.

130. Na ikiwa hapana budi kabisa nawaachane kama Aya ya 130 inavyosema. Ukimwacha wewe hatakuwa kaachwa na Mungu; atampata aliye bora kuliko wewe.

131. Hapana jambo bora kabisa kuliko kumcha Mungu: (a) Kujiepusha na kila Alichokukataza, kwani ni

السموت وما في الارض وكان الله غنيا حميدا ﴿١٣١﴾

vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini, na Mwenyezi Mungu ni Mkwasi na Mwenye kusifiwa.

ولله ما في السموت وما في الارض وكفى بالله وكيلا ﴿١٣٢﴾

132. Na vyote vilivyomo mbinguni na vilivyomo ardhini ni vya Mwenyezi Mungu; na Mwenyezi Mungu anatosha kuwa mlinzi (wa waja Wake. hawamhitajii mwingine).

ان يشا يذهبكم ايها الناس ويات باخرين وكان الله على ذلك قديرا ﴿١٣٣﴾

133. Akitaka atakuondoeni enyi watu, na awalete wengine; na Mwenyezi Mungu ni Muweza wa hayo.

من كان يريد ثواب الدنيا فعند الله ثواب الدنيا والاخرة وكان الله سميعا بصيرا ﴿١٣٤﴾

134. Anayetaka malipo ya dunia (naayatake kwa Mwenyezi Mungu pia) kwani yako kwa Mwenyezi Mungu malipo ya dunia na ya Akhera. Na Mwenyezi Mungu ni Mwenye kusikia (na) Mwenye kuona.

يايها الذين امنوا كونوا قومين بالقسط شهداء لله ولو على انفسكم او الولدين والاقربين ان يكن غنيا او فقيرا فالله اولى بهما فلا تتبعوا الهوى ان تعدلوا وان تلوا او تعرضوا فان الله كان بما تعملون خبيرا ﴿١٣٥﴾

135. Enyi mliomini! Kuweni wenye kusimamisha uadilifu, mtowao ushahidi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu; ijapokuwa ni juu ya nafsi zenu, au (juu ya) wazazi (wenu) na jamaa (zenu). Akiwa tajiri au masikini (wewe usitazame). Mwenyezi Mungu anawastahikia zaidi (kuliko wewe). Basi msifuate matamanio mkaacha kufanya uadilifu. Na kama mkipotoa (shahada) au mkajitenga (na kushuhudia, Mwenyezi Mungu atakuteseni); na Mwenyezi Mungu anazo khabari za yote mnayoyatenda.

يايها الذين امنوا امنوا بالله ورسوله والكتب الذي نزل على رسوله والكتب الذي انزل من قبل ومن يكفر بالله وملئكته وكتبه ورسله واليوم الاخر فقد ضل ضللا بعيدا ﴿١٣٦﴾

136. Enyi mlioamini! Mwaminini Mwenyezi Mungu na Mtume wake na Kitabu alichokiteremsha juu ya Mtume wake, na Vitabu alivyoviteremsha zamani. Na mwenye kumkanusha Mwenyezi Mungu na Malaika wake na Vitabu vyake na Mitume wake na siku ya mwisho, basi bila shaka amepotea upotofu (upotevu) ulio mbali (na haki).

---

salama yako mwenyewe duniani na Akhera; na (b) Kufanya kila unachokiweza katika Alichokuamrisha, kwani ni nafuu yako duniani na Akhera. Uma zote zimeusiwa haya.

132. Mwenyezi Mungu anabainisha kila wakati kuwa hakuna mwenye amri mbele ya Mwenyezi Mungu, la mbinguni wala ardhini. Na anatosha kuwalinda mwenyewe waja Wake wasifikwe na lo lote. Lakini viumbe hawasikii tu. Watatafuta Pepo wa Fulani awalinde au Mzimu au Kaburi au Pango na kama haya. Uko wapi Uislamu wao watu hao?

134. Tunahimizwa tutafute yote mawili—dunia na Akhera.

135. Hapana cha kuleta raha kubwa na masikilizano duniani kama Insafu—Kutimiziana haki. Basi hapa inahimizwa kweli kweli kusimamia haki vilivyo kweli kweli, japokuwa kusimamia huko kutawadhuru wako na kutakkudhuru wewe mwenyewe nafsi yako. Isaidie haki itande, itapakae kila upande.

136. Na hii ni moja katika Aya nyingi zinazowakataza Waislamu kuwaitakidi wanaojidaia Utume baada ya Nabii Muhammad. Hao ni makafiri, na wanaowaitakidi ni makafiri vile vile. Waislamu wote juu yao kufuata Qurani na Hadithi za Mtume. Na zote zimekwisha kusema kuwa Itikadi hiyo ni ukafiri. Na kafiri ni wa Motoni milele. Juu yetu sisi katika kuwajibu wapotezi hao wakituonyesha ya uwongo. wao—tuwaonyeshe Aya hizi za Qurani. Hatutaacha maneno ya Qurani kwa ajili ya maneno ya fulani kama kusema kwao:- "Sheikh Fulani kasema . . ." Ni uwongo tu huo. Hakuwashindi watu hao kuwasingizia mashekhe, kuwa "Sheikh kasema hivi"; na hali ya kuwa ni uwongo kabisa; ni uzushi tu wanaowazulia. Qurani yote inasema *"Min Qablika"*—waliopewa

137. Hakika wale walioamini, kisha wakakufuru, kisha wakaamini, kisha wakakufuru, tena wakazidi ukafiri, Mwenyezi Mungu hatawasamehe wala hatawaongoza njia (ya kheri).

إِنَّ الَّذِينَ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ آمَنُوا ثُمَّ كَفَرُوا ثُمَّ
ازْدَادُوا كُفْرًا لَّمْ يَكُنِ اللَّهُ لِيَغْفِرَ لَهُمْ
وَلَا لِيَهْدِيَهُمْ سَبِيلًا ﴿١٣٧﴾

138. Waambie wanafiki kwamba watapata adhabu inayoumiza

بَشِّرِ الْمُنَافِقِينَ بِأَنَّ لَهُمْ عَذَابًا أَلِيمًا ﴿١٣٨﴾

139. (Wanafiki) ambao huwafanya makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Je! Wanataka wapate utukufu kwao? Basi utukufu wote ni wa Mwenyezi Mungu. (Hauko katika mkono wa mtu).

الَّذِينَ يَتَّخِذُونَ الْكَافِرِينَ أَوْلِيَاءَ مِن دُونِ الْمُؤْمِنِينَ
أَيَبْتَغُونَ عِندَهُمُ الْعِزَّةَ فَإِنَّ الْعِزَّةَ لِلَّهِ جَمِيعًا ﴿١٣٩﴾

140. Naye amekwisha kuteremshieni katika Kitabu (hiki) ya kwamba mnaposikia Aya za Mwenyezi Mungu zinakataliwa na kufanyiwa stihzai, basi msikae pamoja nao, hata waingie katika mazungumzo mengine. (Mtakapokaa) mtakuwa kama wao. Hakika Mwenyezi Mungu atawakusanya wanafiki na makafiri wote pamoja katika Jahannamu

وَقَدْ نَزَّلَ عَلَيْكُمْ فِي الْكِتَابِ أَنْ إِذَا سَمِعْتُمْ
آيَاتِ اللَّهِ يُكْفَرُ بِهَا وَيُسْتَهْزَأُ بِهَا فَلَا تَقْعُدُوا
مَعَهُمْ حَتَّىٰ يَخُوضُوا فِي حَدِيثٍ غَيْرِهِ إِنَّكُمْ إِذًا
مِّثْلُهُمْ إِنَّ اللَّهَ جَامِعُ الْمُنَافِقِينَ وَالْكَافِرِينَ فِي
جَهَنَّمَ جَمِيعًا ﴿١٤٠﴾

---

Utume kabla ya Nabii Muhammad ndio Mitume wa haki, sio wanaojisingizia baada ya kuja Nabii Muhammad.

137. Wamempinga Mtume dhahir shahir katika Aya waliyoifanya ya 138 wakasema: "Wako watu wanaosema ya kuwa, kama mtu anaacha dini baada ya kuamini, basi kufuru yake hii inamstahilishia kupata adhabu ya kuuawa. Lakini Aya hii inavunja kabisa wazo la namna hii . . ."

Wanajua kwa yakini kuwa kauli hiyo hawakuitoa watu, bali kaitoa Mwenyewe Mtume. Na Maimamu wa Hadithi wote wameitaja Hadithi hiyo inayosema: *"Man Baddala Dynahuu Faqtuluuhu"* (Anayebadilisha dini yake ya Uislamu muuweni).

(1) Imam Al Bukhary ameitaja mahala 4: (1) katika *Kitabu Maghazy*, katika mlango wa 60; (2) katika *Kitabud Diyat*, katika mlango wa 6; (3) katika *Kitabus Stitaabatil Murtaddyn*, katika mlango wa 2; (4) katika *Kitabul Ahkam*, katika mlango wa 12.

(2) Imam Muslim ameitaja mahala 3: (1) katika *Kitabul Qasaama* katika Hadithi ya 25 na 26; (2) katika *Kitabul Amaara*, katika Hadithi ya 15.

(3) Imam Abu Daud ameitaja mahala katika *Kitabul Huduud*, katika Hadithi ya 1.

(4) Imam Attirmidhy ameitaja mahala 3: (1) katika *Kitabul Diyaat* katika mlango wa 6; (2) katika *Kitabul Huduud*, katika mlango wa 25; (3) katika *Kitabul Fitan*, katika mlango wa 1.

(5) Imam An Nasaiy ameitaja mahala 5: (1) katika *Kitabu Tahrymid Dam*, katika mlango wa 5, 11 na 14; (2) katika *Kitabul Qasaama*, katika mlango wa 6 na 15.

(6) Imam Ibn Majah ameitaja mahala 2 katika *Kitabul Huduud* katika mlango wa 1 na 2.

(7) kImam Malik ameitaja mahala 1 katika *Kitabul Aqdhiya*, katika Hadithi ya 1.

(8) Imam Ahmad bin Hambal ameitaja mahala 11: (1) katika Juzuu ya kwanza katika sahifa: 217, 282 (mara 2), 322, 382, 409, 430, 444, na 464; (2) katika Juzuu ya tano, katika sahifa 231; (3) katika Juzuu ya sita, katika sahifa 58.

(9) Imam Abu Daudit Tayalisy ameitaja mahala 1 katika Hadithi ya 2689.

Na wengineo. Basi hawazijui Hadithi hizi, nao wamevitaja baadhi ya vitabu hivi mwanzo wa tafsiri yao? Wanazijua Hadithi hizi lakini basi tu wanataka kuwapoteza Waislamu wasiyafuate maneno ya Mwenyezi Mungu wala ya Mtume Wake.

Bali hata huyo mwenye *Ruuhul Maany* — wanayemtaja mara kwa mara—kasema katika sahifa 154 ya Juzuu ya 5 ya hii tafsiri yake kuwa huyo Murtaddi mara tatu za mwanzo huendewa akasemezwa, akatolewa mushkil wake. Ama mara ya 4 huuawa tu. Wameyaona humo haya, lakini basi; hamu ya kuwapoteza Waislamu imewashika.

139. Unakaririwa ubaya wa wanafiki.

140. Kama ilivyokatazwa kusema na kufanya mabaya ndivyo ilivyokatazwa kutazama hayo mabaya yanapofanywa na kuyasikiza yanaponenwa.

141. (Wanafiki) ambao wanakungojeni (mpate msiba): basi mkipata kushinda kunakotoka kwa Mwenyezi Mungu, husema (kukwambieni): "Je! Hatukuwa pamoja nanyi?" (Na kama makafiri wamepata sehemu (ya kushinda) husema: (kuwaambia makafiri), "Je, hatukukurubia kukushindeni (tulipokuwa katika jeshi la Waislamu), tukakuzuilieni na (kudhuriwa na hao) Waislamu?" Basi Mwenyezi Mungu atahukumu baina yenu siku ya Kiyama. Na Mwenyezi Mungu hatawajaalia makafiri njia ya kuwashinda Waislamu (kabisa kabisa mpaka waiondeshe dini yao. Hawatajaaliwa kupata hayo).

الذين يتربصون بكم فإن كان لكم فتح من الله
قالوا ألم نكن معكم وإن كان للكافرين
نصيب قالوا ألم نستحوذ عليكم ونمنعكم من
المؤمنين فالله يحكم بينكم يوم القيامة ولن
يجعل الله للكافرين على المؤمنين سبيلا (١٤١) ع

142. Wanafiki hutaka kumdanganya (hata) Mwenyezi Mungu. Naye atawaadhibu kwa sababu ya kudanganya kwao (huko). Na wanaposimama kusali husimama kwa uvivu, wanaonyesha watu (kuwa wanasali) wala hawamtaji Mwenyezi Mungu ila kidogo

إن المنافقين يخادعون الله وهو خادعهم وإذا
قاموا إلى الصلاة قاموا كسالى يراءون الناس
ولا يذكرون الله إلا قليلا (١٤٢)

143. Wanayumbayumba baina ya huku (kwa Waislamu na huko kwa makafiri). Huku hawako wala huko hawako. Na ambaye Mwenyezi Mungu amemhukumu kupotea, huwezi kumpatia njia (ya kuhisabika kuwa mwongofu).

مذبذبين بين ذلك لا إلى هؤلاء ولا إلى
هؤلاء ومن يضلل الله فلن تجد له
سبيلا (١٤٣)

144. Enyi mlioamini! Msiwafanye makafiri kuwa marafiki badala ya Waislamu. Mnataka awe nayo (Mtume wa) Mwenyezi Mungu hoja dhahiri juu yenu (ya kuwa nyinyi wabaya)?

يا أيها الذين آمنوا لا تتخذوا الكافرين
أولياء من دون المؤمنين أتريدون أن تجعلوا
لله عليكم سلطانا مبينا (١٤٤)

145. Bila shaka wanafiki watakuwa katika tabaka ya chini kabisa katika moto. Hutamkuta kwa ajili yao msaidizi (yo yote)

إن المنافقين في الدرك الأسفل من النار
ولن تجد لهم نصيرا (١٤٥)

146. Isipokuwa wale waliotubu (baada ya unafiki wao) na wakajitengezea na wakamshika Mwenyezi Mungu na wakaukhalisisha utii wao kwa Mwenyezi Mungu, basi hao wako pamoja na Waislamu. Na Mwenyezi Mungu atawapa ujira mkuu (Thawabu kubwa) Waislamu.

إلا الذين تابوا وأصلحوا واعتصموا بالله
وأخلصوا دينهم لله فأولئك مع المؤمنين
وسوف يؤت الله المؤمنين أجرا عظيما (١٤٦)

---

Ikitokea katika majilisi ulioko kufanywa baya au kusimuliwa; kataza. Wakitosikia ondoka wende zako. Mwenyezi Mungu aliwambia katika Aya ya 69 ya *Suratil An-am* amri hii ya kuondoka yanaposemwa mabaya. Wakawa wengine hawajafuata. Ndiyo anawakumbusha tena katika hii Aya ya 140 ya *Suratin Nisaa*.

142. Wanafiki walikuwa wakijitia pamoja na Waislamu katika mambo yao yote ili wasipate kutambulikana kuwa wao wanafiki. Lakini walikuwa hawayaonei raha; wanafanya kwa kuwa hawana budi tu. Wao wanachunga manufaa yao ya kidunia tu—yakiwa kwa makafiri au kwa Waislamu; hawako huku wala hawako huko.

144. Wanakatazwa Waislamu kuwafanya marafiki hao wanafiki.

145. Inatajwa kuwa adhabu yao itakuwa zaidi kuliko makafiri kwani dhara yao kubwa zaidi.

146. Kwenye Aya hii walioifanya kuwa ni ya 147 wameandika hivi: "*Ma'a* hii ndiyo kama ile iliyotumiwa